# UCHUMI WETU

TOLEO NA. 02, OKTOBA 2025








# KUTOKA MEZA YA GAVANA



**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

Ninayo furaha kubwa kuwaletea wasomaji wetu toleo la pili la Jarida la UCHUMI WETU linalotolewa na Benki Kuu ya Tanzania kila robo mwaka. Jarida hili linalengo la kuwafahamisha wananchi matukio muhimu na taarifa sahihi za mwenendo wa uchumi, shughuli zilizotekelezwa na Benki Kuu pamoja na taasisi nyingie za fedha katika robo tatu ya mwaka 2025 na mwelekeo wa robo ya nne ya mwaka huu.

Ni jambo la kujivunia kwamba uchumi wa dunia unaendelea kuimarika licha ya changamoto mbalimbali zinazoathiri kasi na mwenendo wa ukuaji wake. Baadhi ya changamoto hizo ni athari za janga la UVIKO-19, vita vinavyoendelea nchini Ukraine na Mashariki ya Kati, mabadiliko ya tabianchi, kubadilika kwa sera za Marekani kulikosababisha kuadimika kwa fedha za kigeni hasa Dola ya Marekani na kuongezeka kwa ushuru wa forodha.

Hata hivyo, kutokana na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na nchi mbalimbali, uchumi wa dunia na wa kanda zetu za EAC na SADC umeendelea kuimarika na unatarajiwa kukua zaidi katika siku zijazo. Uchumi wa Tanzania Bara katika robo ya kwanza ya mwaka 2025, ulikua kwa asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Mwenendo huu ulichangiwa zaidi na shughuli za uchimbaji wa madini, kilimo, huduma za fedha na bima, shughuli za ujenzi, na uzalishaji viwandani. Aidha, lengo la ukuaji wa uchumi wa asilimia 6.0 katika la mwaka 2025 linatarajiwa kufikiwa kama ilivyopangwa kutokana na uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji pamoja na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti.

Kwa upande wa Zanzibar, uchumi ulikua kwa asilimia 6.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2025, sawa na ukuaji uliorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huu ulichangiwa na shughuli za utalii, ujenzi na kilimo. Vile vile, matarajio ni kufikia ukuaji wa asilimia 7.3 kwa mwaka 2025 kama ilivyopangwa awali kutokana na uwekezaji unaoendelea, shughuli za utalii na ujenzi wa miundombinu.

Kuhusu mwenendo wa sera ya fedha, Benki Kuu ilitekeleza kiwango cha riba ya asilimia 6.0 katika robo ya kwanza na ya pili, na baadaye ilipunguza kiwango cha riba hadi asilimia 5.75 kwa robo ya tatu na ya nne ya mwaka 2025. Uamuzi huu unalenga kudhibiti mfumuko wa bei katika wigo wa asilimia 3 hadi 5 ili kuendelea kulinda thamani ya shilingi yetu na kusaidia ustawi wa uchumi wa taifa.

Aidha, utekelezaji wa sera ya fedha katika kila robo mwaka ulihakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha kwenye uchumi, kupunguza riba ya mikopo ya siku 7 baina ya mabenki na kuongeza ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ambapo iliongeza shughuli za kiuchumi nchini.

Jarida hili la UCHUMI WETU limetambua pia mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha robo ya tatu, ambapo Benki Kuu ya Tanzania imepata tuzo kadhaa zenye heshima kubwa ndani na nje ya nchi. Miongoni mwa tuzo hizo ni ile ya Ubunifu katika Huduma Jumuishi za Fedha, inayotolewa na Jumuiya ya Kimataifa ya Huduma Jumuishi za Fedha (Alliance for Financial Inclusion - AFI) yenye nchi wanachama 84 duniani. Tuzo hii mashuhuri inalenga kutambua juhudi za nchi zinazofanya vizuri zaidi katika ubunifu, matumizi ya teknolojia, na uongozi imara katika kuongeza kasi ya upatikanaji na matumizi ya Huduma Jumuishi za Fedha.

Benki Kuu imeibuka kidedea kufuatia utekelezaji madhubuti wa mfumo wa malipo ya papo kwa papo yaani TIPS ambao umesaidia kupunguza gharama kwa wananchi na kurahisisha upatikanaji wa huduma za fedha kwa njia ya kidigitali muda wote na mahali pote nchini. Vile vile, Benki Kuu imeonesha mafanikio katika matumizi ya msimbo milia wa malipo (QR Code) unaofahamika kama TANQR unaowezesha wafanyabiashara kupokea malipo kwa urahisi kutoka benki na kampuni za simu. Mafanikio haya yamewezesha ongezeko la miamala kwa mwaka 2024/25 kufikia milioni 560 yenye thamani ya shilingi trilioni 41; pamoja na miamala ya kutumia msimbo milia na Lipa Namba milioni 60 yenye thamani ya shilingi trilioni 4.

Tuzo nyingine ni ya Mshindi wa Kwanza wa Taasisi za Umma kwa Utawala Bora na Uwajibikaji iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa Mkutano wa viongozi wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa mwaka 2024/25.

Vile vile, Benki Kuu ilifanikiwa kupokea tuzo nyingine katika maonesho mbalimbali kuhusu utoaji wa elimu ya fedha na uwekezaji pamoja na tuzo ya kuchangia ujenzi wa miundombinu ya kudumu katika maonesho ya madini Geita. Tuzo hizi ni kielelezo cha ari, weledi na kujituma kwa wafanyakazi wote wa Benki Kuu katika kutimiza majukumu yao kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Jambo lingine lililopewa umuhimu katikia toleo hili ni uzinduzi wa Mfumo Mkuu wa Kibenki Jumuishi (Integrated Central Banking System – iCBS), ambapo Tanzania imekuwa nchi ya kwanza Afrika kutengeneza mfumo huo kwa kutumia wataalamu wa ndani ya Benki Kuu. Hatua hii ni ya kujivunia kwa kuwa inaongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kibenki na kupunguza gharama kubwa ambazo zingetumika endapo ungenunuliwa au kutengenezwa na wataalamu wa nje. Mfumo huu ni ushahidi wa uwezo mkubwa wa wataalamu wetu wa ndani na dhamira ya Benki Kuu ya Tanzania kuendelea kutumia teknolojia, bunifu na vipaji vya watumishi wazalendo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Katika kipindi hiki, Benki Kuu imezindua Makumbusho ya Benki Kuu ya Tanzania yaliyopo katika Makao Makuu Ndogo jijini Dar es Salaam. Makumbusho haya yanahifadhi historia ya fedha na sarafu za Tanzania, mabadiliko ya mifumo ya kifedha na kumbukumbu muhimu za kiuchumi na sekta ya fedha nchini. Hivyo, napenda kuwakaribisha wadau wote wakiwemo wanafunzi, watafiti, watalii na wananchi wote kutembelea makumbusho haya ili kujifunza zaidi kuhusu historia na matukio muhimu ya Benki Kuu katika kutekeleza sera ya fedha, kusimamia uthabiti wa sekta ya fedha na kuimarisha uchumi wa taifa letu.

Nina imani kuwa kupitia jarida hili la UCHUMI WETU, wasomaji wataendelea kupata uelewa mpana wa shughuli za Benki Kuu, na taarifa sahihi kuhusu uthabiti wa sekta ya fedha na mwelekeo wa uchumi wa Tanzania. Karibuni wote ili kusoma, kujifunza na kushirikiana nasi katika safari ya kujenga uchumi imara na shindani.

**Emmanuel Mpawe Tutuba**
Gavana,
Benki Kuu ya Tanzania



# KUTOKA MEZA YA MHARIRI MKUU



**Ndugu Wasomaji,**

Karibuni katika toleo la pili la Jarida la Uchumi Wetu ambalo limesheheni mambo mbalimbali ambayo Benki Kuu ya Tanzania inayafanya, kuyasimamia na kuratibu na yale yanayohusiana na shughuli zake kwa maslahi mapana ya uchumi wa nchi yetu.

Katika toleo hili, tumekuletea habari zinazohusu shughuli mbalimbali ambazo Benki Kuu imezifanya katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2025/2026 ikiwemo; Uzinduzi wa Mfumo Mkuu Jumuishi wa Kibenki (iCBS) ambao unachocheo huduma bora na zenye ufanisi za kibenki pamoja na uzinduzi wa kikokotoo cha riba cha Benki Kuu ambacho kinampa faida mwananchi kufahamu riba kabla ya kukopa katika taasisi za kifedha.

Mengine utakayoyapata ni pamoja na shughuli mbalimbali zinazofanywa na matawi ya Benki Kuu ambapo kwa upana wake tumeliangalia Tawi la Mbeya katika toleo hili. Pia tumeangazia kwa kina masuala ya kimataifa yenye athari za moja kwa moja katika uchumi wetu.

Kwa kutambua kuwa, Benki Kuu siyo kisiwa bali inashirikiana na taasisi nyingine, tumekuletea makala kutoka mamlaka nyingine za usimamizi na udhibiti zikiwamo Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Bima (TIRA) na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ili kukuletea msomaji taarifa kamili zihusuzo uchumi kama lilivyo jina la Jarida letu pendwa 'Uchumi Wetu'.

Karibuni sana wasomaji wetu.

**Victoria Msina**
Meneja, Idara ya Mawasiliano
Benki Kuu ya Tanzania.

# RIBA YA BENKI KUU KUENDELEA KUWA ASILIMIA 5.75



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki Tanzania, Bw. Theobald Sabi, akizungumza katika mkutano wa kutangaza Riba ya Benki Kuu uliofanyika tarehe 2 Oktoba, 2025 kwenye ofisi za BoT, jijini Dar es Salaam.



Gavana, Bw. Emmanuel Tutuba akizungumza na waandishi wa habari na viongozi wa mabenki na taasisi za fedha katika mkutano wa kutangaza Riba ya Benki Kuu kwa robo ya 4 ya mwaka. Mkutano huo ulifanyika tarehe 2 Oktoba, 2025 katika ofisi za BoT, jijini Dar es Salaam.

Kamati ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeamua kuendelea na kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) cha asilimia 5.75 kwa robo ya nne ya mwaka 2025 kama ilivyokuwa kwa robo ya tatu iliyoishia mwezi Septemba 2025.

Kiwango cha Riba cha Benki Kuu (CBR) ni kiwango kinachowekwa na BoT kama rejea katika utekelezaji wa shughuli zake mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kukopesha benki za biashara. Kiwango hiki huathiri riba za mikopo baina ya benki za biashara, ambazo zinapaswa kuwa ndani ya wigo wa ±2.0% ya CBR iliyowekwa.

Akizungumza katika mkutano na viongozi wa benki, taasisi za fedha na waandishi wa habari uliofanyika tarehe 2 Oktoba 2025, Gavana wa BoT ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Sera ya Fedha, Bw. Emmanuel Tutuba, alisema uamuzi huu unatokana na makadirio ya Benki Kuu yanayoonesha kuwa uchumi utaendelea kukua na mfumuko wa bei utabaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5 .

'Uamuzi wa kutokubadili Riba hii umetokana na tathmini iliyofanyika kuhusu mwelekeo wa mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi. Mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.4 mwezi Agosti, na unatarajiwa kubakia, ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Wakati huohuo, makadirio ya BoT yanaonesha kuwa uchumi utaendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha", Amesema.

Aliongeza kuwa utekelezaji wa sera ya fedha katika robo ya tatu ya mwaka ulifanikiwa kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha kwenye uchumi ambapo ilipelekea kupungua kwa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya mabenki.

"Benki Kuu ilitumia nyenzo zake za sera ya fedha, hususan mikopo ya muda mfupi kwa mabenki (reverse repo operations) kuongeza ukwasi kwenye uchumi. Kufuatia hatua hii, hali ya ukwasi iliimarika na kupelekea kupungua kwa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya mabenki". Ameeleza Gavana Tutuba.

Kuhusu mwenendo wa uchumi nchini, Gavana alisema uchumi wa Tanzania Bara ulikua kwa asilimia 5.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2025, ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Mwenendo huu ulichangiwa zaidi na shughuli za uchimbaji madini, kilimo, huduma za fedha na bima, ujenzi, na shughuli za uzalishaji viwandani.

Kwa upande wa Zanzibar, alieleza kuwa uchumi ulikua kwa asilimia 6.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2025, sawa na ukuaji uliorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za utalii, ujenzi na kilimo.

Naye, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki nchini (TBA), Bw. Theobald Sabi, alisema kuwa ukuaji wa pato la taifa, kuongezeka kwa ukwasi wa fedha za kigeni, kuimarika kwa thamani ya shilingi pamoja na ufanisi wa sekta mbalimbali za uchumi ikiwemo utalii, madini na kilimo, ni viashiria vinavyothibitisha uimara na uhimilivu wa uchumi wa Tanzania.



# MUHTASARI WA TAARIFA YA KAMATI YA SERA YA FEDHA KWA ROBO YA NNE YA MWAKA 2025

**RIBA YA BENKI KUU KWA ROBO YA NNE YA 2025 KUBAKIA 5.75%**




### UKUAJI WA UCHUMI

**Tanzania Bara:**
Ulikua kwa 5.4% robo ya kwanza 2025, ikilinganishwa na 5.2% kipindi hicho 2024

### UKUAJI WA MALIPO YA KAWAIDA

**Tanzania Bara:**
Nakisi ilipungua hadi 2.4% ya Pato la Taifa mwaka ulioishia Septemba 2025, kutoka 3.8% mwaka uliotangulia.

**Zanzibar:**
Ilipanda hadi dola milioni 685.6 mwaka ulioishia Septemba 2025, kutoka milioni 499.0 mwaka uliotangulia.

### SEKTA YA KIBENKI

Mikopo chechefu iliendelea kupungua hadi 3.3% mwezi Agosti 2025, chini ya kiwango kinachohimilika cha 5%

### MFUMUKO WA BEI

**Tanzania Bara:**
Ulikuwa 3.4% mwezi Agosti 2025, ndani ya lengo la nchi la 3 hadi 5%

**Zanzibar:**
Ulipungua kutoka 4.2% hadi 4% na kubakia ndani ya lengo

### AKIBA YA FEDHA ZA KIGENI

Mwishoni mwa Septemba 2025 ilifikia dola bilioni 6.7, ikitosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa zaidi ya miezi 5.

### UJAZI WA FEDHA

Ulikua kwa wastani wa 20.4% kwa robo ya tatu ya mwaka 2025, ikilinganishwa na 19.1% katika robo iliyotangulia.



# BOT YANG'ARA ANGA ZA KIMATAIFA KWA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA



Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania anayesimamia Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Bi. Sauda Msemo, akiwa ameshika Tuzo Kuu ya Ubunifu katika Huduma Jumuishi za Fedha (Nestor Espenilla Jr. Financial Inclusion Innovation Award) ambayo Benki Kuu ilitunukiwa katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Huduma Jumuishi za Fedha uliofanyika Swakopmund, Namibia mwanzoni mwa mwezi Septemba 2025.

Benki Kuu ya Tanzania imetunukiwa Tuzo Kuu ya Ubunifu katika Huduma Jumuishi za Fedha (Nestor Espenilla Jr. Financial Inclusion Innovation Award) inayotolewa na Jumuiya ya Huduma Jumuishi za Fedha (AFI) yenye nchi wanachama 84.

Tuzo hii mashuhuri inalenga kutambua nchi wanachama wa AFI ambazo zimeonesha juhudi kubwa katika ubunifu na matumizi ya teknolojia, pamoja na kutambua uongozi imara katika kuchochea kasi ya upatikanaji na matumizi ya Huduma Jumuishi za Fedha.

Tuzo hiyo ilipokelewa na Naibu Gavana anayeshughulikia Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Bi. Sauda Msemo, kwa niaba ya Gavana wa Benki Kuu, Bw. Emmanuel Tutuba, wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Huduma Jumuishi za Fedha uliofanyika mjini Swakopmund, nchini Namibia. Bi. Msemo aliongoza ujumbe wa Benki Kuu ulioshiriki katika mikutano hiyo kama wawakilishi wa vikundi kazi na kamati za AFI.

Baadhi ya mambo yaliyoiwezesha Benki Kuu kuibuka kidedea ni utekelezaji madhubuti wa Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Papo (TIPS); kuanzishwa kwa mazingira ya majaribio ya ubunifu (Bank of Tanzania Fintech Regulatory Sandbox Regulations, 2024); mfumo wa kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi (SEMA na BoT); pamoja na matumizi ya msimbo milia wa malipo (QR Code) ujulikanao kama TANQR.

Kwa mujibu wa takwimu za BoT, katika mwaka wa fedha 2024/25, mfumo wa TIPS ulisajili zaidi ya miamala milioni 560 yenye thamani ya shilingi trilioni 41, huku miamala ya msimbo milia (QR Code) na Lipa Namba ikifikia zaidi ya milioni 60 yenye thamani ya shilingi trilioni 4.

Aidha, Meneja wa BoT wa Idara ya Huduma Jumuishi za Fedha, Bi. Nangi Massawe ametambuliwa kupitia Tuzo za Uongozi wa Kiufundi za AFI (AFI Technical Leadership Awards). Tuzo hizi hutolewa kwa wataalamu kutoka nchi wanachama wa AFI ambao wameonyesha mchango mkubwa wa kiufundi, ushiriki wa hali ya juu katika kubadilishana maarifa, na kutoa mafunzo kwa nchi wanachama wengine ili kukuza ujumuishaji wa kifedha kupitia sera, mikakati na ubunifu wa kitaifa.

Vilevile, katika mkutano huo, Meneja Msaidizi wa BoT wa Idara ya Huduma Jumuishi za Fedha, Bw. Melvin Kilemile, alihitimu programu za mafunzo ya uongozi wa Huduma Jumuishi za Fedha kutoka Chuo cha Uongozi wa Huduma Jumuishi za Fedha cha Fletcher. Aidha, Mchambuzi Mwandamizi wa Masuala ya Fedha, Bw. Dastan Massawe, alikuwa miongoni mwa wahitimu wa kundi la kwanza la programu ya kuwaandaa vijana kwa nafasi za uongozi katika huduma jumuishi za fedha.

Mafanikio haya ni kielelezo cha uongozi thabiti wa Benki Kuu chini ya Gavana Emmanuel Tutuba katika kusimamia juhudi za kuongeza na kuchochea matumizi ya huduma za fedha kwa kutumia teknolojia. Hatua hizi zinalenga kuongeza ufanisi, kupunguza gharama, na kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanashiriki kikamilifu katika maendeleo ya uchumi wa taifa na kuboresha maisha yao.



Mkurugenzi wa Mifumo ya Malipo ya Taifa wa Benki Kuu, Bi. Lucy Shaidi akiwa ameshika tuzo Tuzo Kuu ya Ubunifu katika Huduma Jumuishi za Fedha katika Mkutano na Waandishi wa Habari uliofanyika tarehe 16 Septemba 2025. Katika mkutano huo Bi. Lucy aliwaeleza kuwa Benki Kuu imeibuka kidedea kufuatia utekelezaji Madhubuti wa Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Hapo (TIPS) na namna ambavyo umesaidia kupunguza gharama kwa wananchi kufanya miamala kwa njia ya kidijitali.

# RAIS SAMIA ATOA RAI WATANZANIA KUSHIRIKI UTEKELEZAJI DIRA YA MAENDELEO 2050




Hatimaye Tanzania tuitakayo miaka 25 ijayo imewekwa bayana kupitia uzinduzi wa Dira ya Maendeleo 2050.

Akizindua dira hiyo jijini Dar es Salaam tarehe 17 Julai 2025, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alitoa wito kwa Watanzania kushiriki katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ili kufikia lengo kuu la kujenga Taifa jumuishi, lenye ustawi, la haki na linalojitegemea.

Dira hiyo imeweka vipaumbele katika sekta tisa ambazo ni kilimo, viwanda, ujenzi, madini, utalii, uchumi wa buluu, huduma za kijamii, huduma za kifedha, na michezo na ubunifu.

Rais Samia alisema Dira 2050 ni matokeo ya mchakato jumuishi uliohusisha maoni ya wananchi na wadau wote na inalenga kufanikisha maendeleo jumuishi kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Aliongeza kuwa Dira hiyo iliyozingatia matarajio ya Watanzania imejengwa juu ya msingi wa mafanikio na mafunzo ya historia ya maendeleo ya Tanzania tangu Uhuru, ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto za utekelezaji wa Dira ya 2025.

"Maudhui ya Dira 2050 yametokana na maoni na matakwa ya Watanzania wenyewe. Tumefikiri wenyewe, tumeandika wenyewe, tumepanga wenyewe na tutatekeleza wenyewe," alisema Rais Dkt. Samia.

Kuhusu uandaaji wa Dira, Rais Dkt. Samia alisema kuwa umezingatia muktadha wa sasa wa dunia unaogusa masuala muhimu kama vile mabadiliko ya mfumo wa uchumi wa dunia, mabadiliko ya tabianchi, ongezeko kubwa la vijana nchini na mapinduzi ya kiteknolojia.

"Ukubwa wa rasilimali, ari na uwezo wa wananchi, Tanzania ina kila sababu ya kuweka na kufikia malengo makubwa ya maendeleo iliyojiwekea, ikiwa ni pamoja na lengo kuu la kuwa nchi ya kipato cha kati cha juu yenye uchumi wa Dola Trilioni Moja ifikapo mwaka 2050,"alisema Rais Samia

Rais Dkt. Samia pia alisisitiza ili kufikia utekelezaji wa Dira 2050, ipo haja ya kufanya mabadiliko ya kifikra, kimtazamo na kimatendo ili kufanikisha malengo yake, akiongeza kuwa utekelezaji wa Dira hiyo unahitaji ushirikiano wa Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, sekta binafsi, jamii, taasisi za dini, mashirika ya kiraia na wananchi mmoja mmoja.

Katika hilo, Rais Dkt. Samia ameielekeza Tume ya Taifa ya Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kuandaa mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na tathmini pamoja na vigezo vya kupima utendaji wa kila taasisi ya umma kwa kila hatua ya utekelezaji.

Vilevile, Rais Dkt. Samia ameziagiza Wizara zote kufanya mapitio ya sera zake ili zishabihiane na Dira hiyo, na Tume ya Kurekebisha Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuanza mchakato wa kupendekeza maboresho ya kisheria yatakayowezesha utekelezaji wa Dira kwa ufanisi.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Samia ameagiza kuandaliwa mkakati mahsusi wa mawasiliano na elimu kwa umma kuhusu Dira 2050 ili kuongeza uelewa na ushiriki wa wananchi, huku akisisitiza uwazi katika utoaji wa taarifa za maendeleo ili kuimarisha uaminifu kati ya Serikali na wananchi.

# iCBS: HATUA MPYA KATIKA USALAMA NA USIMAMIZI WA FEDHA ZA TAIFA

Sekta ya fedha nchini Tanzania imepiga hatua kubwa ya kiteknolojia kupitia uzinduzi wa Mfumo Mkuu Jumuishi wa Kibenki (Integrated Core Banking System – iCBS).

Uzinduzi huo ulioongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango Julai 30, 2025 katika Makao Makuu Ndogo ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Mfumo huu, ambao umetengenezwa na wataalamu wa ndani wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ni wa kwanza wa aina yake barani Afrika na unatajwa kuwa chachu ya mageuzi katika usimamizi wa fedha za taifa.

Akizungumzia hilo, Dkt Mpango alisema kuundwa kwa mfumo wa iCBS kwa kutumia wataalamu wa ndani si tu mafanikio ya kiteknolojia bali uthibitisho wa uhuru uliyopo nchini.

“Hii ni tofauti na kipindi cha nyuma ambapo watoa huduma wa nje waliweka mazingira ya utegemezi wa mifumo ya kidigitali kutoka kwao kwa maana ya ujuzi na vifaa tutoe kwao na wakati wa matengenezo tuwatafute, kwa kutengeneza mfumo huo imejidhihirisha kuwa nchi inaweza kujitegemea,” amesema Dk. Mpango

**Zifuatazo ni faida za kuzinduliwa kwa mfumo huu;**

**Uzalendo wa Kiteknolojia**

Moja ya mambo yanayoufanya iCBS kuwa wa kipekee ni ukweli kwamba umetengenezwa kikamilifu na Watanzania. Kwa kawaida, nchi nyingi hulazimika kununua mifumo kama hii kutoka nje kwa gharama kubwa na masharti ya kuendelea kuilipa kampuni husika kwa matengenezo. Tanzania imevunja mwiko huu kwa kuonyesha kuwa wataalamu wake wana uwezo wa kuunda mfumo mkubwa na nyeti unaohusu uchumi wa taifa.

Hatua hii si tu inaleta heshima kwa nchi, bali pia inalinda usiri wa taarifa za kifedha za serikali na taasisi zake, jambo ambalo mara nyingi hukabiliwa na changamoto endapo huduma hizo zinapewa makampuni ya nje.

**Mhimili wa Malipo Nchini**

iCBS si mfumo wa kawaida. Ni uti wa mgongo wa malipo na utunzaji wa fedha nchini. Kupitia mfumo huu, Benki Kuu inatunza akaunti za serikali zote mbili – Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – pamoja na mashirika ya umma, mabenki ya biashara, washirika wa maendeleo na taasisi nyinginezo.

Pia, mfumo huu unarahisisha malipo ya ndani na nje ya nchi, uchakataji wa taarifa za kifedha na usimamizi wa sarafu. Kwa kuongeza, unajumuisha huduma za kibenki kupitia simu ya mkononi kwa ajili ya watumishi wa Benki Kuu, hatua inayodhihirisha kusogea kwa huduma muhimu karibu zaidi na watumiaji wake.

**Faida kwa Taifa**

Faida za mfumo huu ni nyingi. Kwanza, unalipunguzia taifa mzigo wa gharama za manunuzi na matengenezo kutoka kwa kampuni za nje. Pili, unalinda taarifa nyeti za kifedha ambazo kimsingi hazipaswi kufikishwa kwa watoa huduma wa kigeni. Tatu, unawajengea uwezo wataalamu wa ndani na kuimarisha ujuzi wao katika teknolojia ya kifedha.




Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, akizindua Mfumo Mkuu Jumuishi wa Kibenki (iCBS) wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) katika hafla iliyofanyika BoT jijini Dar es Salaam. Kutokea kulia ni Naibu Gavana, Bw. Julian Banzi Raphael; Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry Silaa; Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Chande; Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba; Waziri wa Fedha Zanzibar, Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum na Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila.



Wageni waalikwa mbalimbali katika halfa ya uzinduzi wa Mfumo Mkuu Jumuishi wa Kibenki (iCBS) katika hafla iliyofanyika BoT jijini Dar es Salaam.

Zaidi ya hayo, mfumo huu unaiweka Tanzania katika ramani ya dunia kama taifa linaloweza kuunda mifumo mikubwa ya kiteknolojia bila kutegemea msaada wa nje. Hii ni hatua muhimu kuelekea kujitegemea na kujiamini kitaifa katika nyanja za kidijitali.

Mfumo Mkuu Jumuishi wa Kibenki (iCBS) ni zaidi ya mfumo wa kiteknolojia. Ni alama ya ubunifu, uzalendo na uthubutu wa Watanzania katika kujenga mifumo ya kitaifa. Kupitia mfumo huu, Tanzania inajihakikishia usalama wa taarifa za kifedha, inapunguza gharama, na kuonesha ulimwengu kwamba Afrika inaweza kusimama yenyewe katika teknolojia ya kifedha.

Kwa hakika, uzinduzi wa iCBS ni somo kwa nchi nyingine barani Afrika kwamba suluhu za ndani zinawezekana endapo rasilimali watu zitathaminiwa na kupewa nafasi ya kuonyesha uwezo wao.

Kwa mafanikio haya, Tanzania imeonesha uwezo mkubwa wa kujitegemea kiteknolojia na kuimarisha sekta ya fedha kwa njia ya ubunifu wa ndani, hatua inayotoa matumaini makubwa kwa maendeleo ya kiuchumi na kidijitali ya taifa.

# RAIS MWINYI: UMEME WA UHAKIKA ZANZIBAR UTACHOCHEA UCHUMI



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi , akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Umeme Zanzibar. Hafla ya uzinduzi wa mradi huo ilifanyika katika Viwanja vya Hoteli ya Verde, Mtoni, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Uimarishaji wa miunfombinu ya umeme visiwani Zanzibar unatajwa kuwa miongoni mwa sababu zitakazochochea ukuaji zaidi wa uchumi.

Hayo yameelezwa na Rais wa Zanzibar Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi Oktoba 1, 2025 katika hafla ya uzinduzi wa mradi wa uboreshaji wa mfumo wa umeme Zanzibar uliofanyika katika Viwanja vya Hoteli ya Verde, Mtoni, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Mwinyi alisema Serikali itaendeleza miradi mbalimbali ya kimkakati katika sekta ya nishati kwa lengo la kuifanya Zanzibar kuwa na umeme wa uhakika na wa kuaminika.

"Hatua hii ni muhimu katika kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kuboresha huduma za umeme kwa wananchi na kuimarisha mazingira ya uwekezaji,"alisema Dkt. Mwinyi.

Kwa mujibu wa Gavana wa Benki Kuu (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba akisoma taarifa ya Riba ya Benki Kuu katika robo ya mwisho yam waka 2025 alisema uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 6.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2025, sawa na ukuaji uliorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huu ulichangiwa na shughuli za utalii, ujenzi na kilimo.




Kuhusu uzinduzi wa mradi huo, Rais Dkt. Mwinyi alisema kuwa ni uthibitisho wa dhamira ya Serikali katika utekelezaji wa ahadi zake kwa wananchi, sambamba na kuondoa changamoto za kukatika kwa umeme, kupungua kwa kiwango cha umeme katika baadhi ya maeneo na kupunguza gharama za uendeshaji.

"Serikali itaendelea kujenga miundombinu mipya ya umeme ikiwemo kuwekeza katika nishati mbadala kupitia jua na upepo, pamoja na kuanzisha mitambo ya usambazaji umeme kwa wananchi.

"Utekelezaji wa mikakati hii unalenga kuhakikisha takribani wananchi 70,000 wanapatiwa huduma ya umeme,"alisema na kuongeza Rais Dkt. Mwinyi
Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Mwinyi amewahakikishia wananchi kuwa Serikali ipo mbioni kushusha gharama za kuunganisha umeme majumbani kutoka TZS 200,000 za sasa hadi kufikia TZS 100,000 pekee.

Vilevile, amefafanua mikakati mingine ikiwemo kuviunganisha visiwa vidogo vya Njau na Kokota na huduma ya umeme, pamoja na kukamilisha mradi mkubwa wa nyaya za umeme wa chini ya bahari (Submarine Power Cable) utakaosambaza nishati kisiwani Pemba.
Dkt. Mwinyi ametoa pongezi kwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Kampuni ya NOVASIS International kwa usimamizi bora na ukamilishaji wa mradi huo kwa wakati, huku akiwataka wananchi na wadau kulinda miundombinu hiyo ili ilete manufaa yaliyokusudiwa, sambamba na kuendelea kusimamia miradi mingine ya kimkakati kwa ufanisi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Bw. Joseph Kilangi, amesema mradi huo uliogharimu Dola za Marekani milioni 8.4 na kukamilika kwake kumeiwezesha Zanzibar kupokea umeme kutoka Tanzania Bara kwa kiwango cha 132 KV badala ya 114 KV kilichokuwapo awali.

# BOT KINARA WA UTAWALA BORA KWA MASHIRIKA YA UMMA



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango akikabidhi Tuzo ya BoT kwa Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba pamoja na Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Dkt. Natu Mwamba.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imetunukiwa tuzo ya mshindi wa kwanza kwa utawala bora katika kundi la mashirika ya kibiashara na yasiyo ya kibiashara.

Hatua hiyo imetajwa kuwa ni uthibitisho wa dhamira yake ya kuendeleza viwango vya juu vya utawala bora, uwazi na uwajibikaji wa taasisi.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango alikabidhi tuzo hiyo iliyotolewa na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, wakati wakati wa hafla ya ufunguzi wa kikao kazi cha Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma kilichofanyika jijini Arusha Agosti 24, 2025.

"Vigezo vilivyotumika katika utoaji wa tuzo hiyo vilijikita katika utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa kiwango cha juu, upatikanaji wa maoni chanya ya ukaguzi, uwazi katika kuchapisha taarifa za kifedha, pamoja na tathmini nzuri ya utendaji wa Bodi ya Wakurugenzi,"alisema Msajili wa Hazina Bw. Nehemia Mchechu

Mafanikio haya ni matokeo ya juhudi za pamoja za menejimenti, wafanyakazi na viongozi wa Benki Kuu katika kutekeleza majukumu yake kwa weledi na kwa manufaa ya Taifa.

Mbali na tuzo hiyo, kikao kazi hiko kilihudhuriwa na zaidi ya Wenyeviti wa Bodi na Wakuu wa Taasisi za Umma 650 jijini Arusha kati ya Agosti 23–26, 2025 na kukubaliana juu ya maazimio tisa yanayolenga kuimarisha ufanisi wa taasisi za umma, kuongeza tija na kupunguza utegemezi kwa Serikali.

Miongoni mwa maazimio hayo ni kuimarisha usimamizi wa rasilimali za umma kwa kudhibiti matumizi na kuongeza ubunifu, pamoja na kusisitiza uwekezaji zaidi katika tafiti ili kusaidia maamuzi yanayotegemea ushahidi wa kitaalamu.

Aidha, taasisi hizo zimekubaliana kufanya mapitio ya sera na sheria zinazosimamia shughuli zao, ili kubaini changamoto zilizopo na kutoa mapendekezo ya maboresho.




Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango akikabidhi Tuzo ya BoT kwa Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba pamoja na Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Dkt. Natu Mwamba. Wa kwanza kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo.

# DKT. MPANGO AWAALIKA WAWEKEZAJI WA MAREKANI NCHINI, ATAJA FAIDA




Makamu wa Rais wa Mhe. Dkt. Philip Mpango amewaalika wawekezaji kutoka nchini Marekani kuwekeza Tanzania huku akipigia chapuo maboresho ya sheria na miundombinu yaliyofanywa katika sekta mbalimbali.

Makamu wa Rais alisema hayo Septemba 23, 2025 wakati akifungua Jukwaa la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Marekani lililofanyika kando ya Kikao cha 80 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA 80) Jijini New York nchini Marekani.

“Serikali ya Tanzania inatambua sekta binafsi ni mshirika mkuu katika juhudi za maendeleo kwa ajili ya mabadiliko ya kijamii na kiuchumi. Tanzania imekuwa na utulivu wa kisiasa na kijamii kwa miaka 60, miundombinu inayoboreshwa kwa kasi huku mazingira ya biashara yakiwa yameboreshwa kwa kiasi kikubwa hivyo wafanyabiashara na wawekezaji wa Marekani wanaweza kutumia fursa hiyo kuwekeza,”alisema Dkt. Mpango

Pia alitoa wito kwa wafanyabiashara wa Tanzania kufikiria na kuchukua hatua kimataifa, kwa kuchangamkia fursa zilizopo katika soko la Marekani.

Dk Mpango aliongeza kuwa Serikali ya Tanzania inafanya kazi kila mara ili kuboresha na kuweka mazingira wezeshi kwa biashara na uwekezaji.
“Tunaboresha mazingira ya uwekezaji ambapo kwa sasa tumepunguza muda wa usajili wa biashara kutoka siku 14 hadi saa 24, Vibali vya uwekezaji vilivyokuwa vikichukua miezi, sasa vinachukua saa au siku kupitia Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi (TISEZA),”alisema Dkt Mpango

Aliongeza kuwa Serikali imedhamiria kuboresha mazingira ya Udhibiti, ikiwa ni pamoja na kuondoa kanuni zisizo za lazima pamoja na kuwekeza katika elimu ili kuzalisha wafanyakazi wenye ujuzi unaohitajika.

Jukwaa la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Marekani limehudhuriwa na wawekezaji na wafanyabiahsara kutoka Tanzania na Marekani ambapo wameipongeza Tanzania kwa uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji pamoja na kuwa na sera zinazotabirika, amani na wananchi wakarimu.

Dkt Mpango aliwaalika wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Marekani kuwekeza nchini Tanzania katika sekta muhimu na za kimkakati zikiwemo madini adimu na muhimu.

"Wakati Marekani inawekeza kwenye nishati safi, Tanzania inasimama kama muuzaji wa kuaminika wa madini ya kimkakati kama vile Graphite yaliyopo Mahenge, mkoani Morogoro, ambayo yanakadiriwa kutoa hadi asilimia 15,” alisema Dk Mpango.

Aliongeza kuwa uwekezaji katika madini unatilia mkazo zaidi katika uongezaji thamani kuanzia uchimbaji madini, usindikaji hadi uzalishaji wa betri.

Pia wawekezaji wa Marekani wamesema malengo ya Dira ya Maendeleo 2050 yakufikia uchumi wa dola Trilioni 1 yanawezekana kutokana na fursa mbalimbali zilizopo.




# WAZIRI MKUU AIPA HEKO DSE KWA UBUNIFU, UKUAJI WA THAMANI

'Hongera Soko la Hisa la Dar es Salaam (DES)' , Kauli hiyo ya pongezi imetolewa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa kutokana na ukuaji na ubunifu unaofanywa na soko hilo.

Mhe. Majaliwa ametoa pongezi hizo Agosti 26, 2025 alipotembelea ofisi za DSE jijini Dar es Salaam huku akitaja ongezeko la thamani ya soko hilo hadi kufikia TZS 21 trilioni Julai mwaka huu.

Amesema kuwa soko hilo limeongeza ukuaji wa mauzo ya hisa kwa zaidi ya asilimia 246 pamoja na ongezeko la idadi ya wawekezaji hadi zaidi ya akaunti 683,000 ikiwa ni ishara ya ukuaji imara wa sekta ya mitaji nchini

Mhe. Majaliwa amesema katika kipindi hicho mauzo ya hatifungani na hatifungani zenye maudhui ya kusaidia mazingira na jamii yalifikia zaidi ya shilingi trilioni 3 hadi kufikia Julai.

"Hiki ni kielelezo cha ubunifu na mchango wa DSE katika kuendeleza uchumi jumuishi na endelevu wa Taifa letu, hii hatuwezi acha ikapita ni lazima tuwapongeze,"alisema Majaliwa.
Akizungumza alipotembelea ofisi za DSE, Mhe. Majaliwa alitangaza kununua hisa zenye thamani ya TZS 100 milioni katika soko la hisa la Dar es Salaam.

"Watanzania wekeni kipaumbele cha kufanya uwekezaji kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam kwa njia ya kidigitali ili kupata fursa ya kuwa sehemu ya kumiliki makampuni na kupata fedha kupitia faida inayotengenezwa na kampuni na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa letu," alisema.

Waziri Mkuu aliiagiza Wizara ya Fedha iendelee kushirikiana na DSE katika kutoa elimu ya fedha kwa wananchi wote ili kuhakikisha fursa zinazotolewa na soko hilo zinanufaisha Watanzania wengi zaidi.

Naye, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Elijah Mwandumbya, alisema ili kufanikisha malengo ya Dira Taifa ya Maendeleo ya 2050 Serikali imeweka mpango wa kuendeleza bidhaa mpya za kifedha kama vile hati fungani, kuimarisha mifumo ya kidijitali katika soko la DSE ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi wakiwemo Diaspora.

Amesema eneo lingine ni kuendeleza ushirikiano na sekta binafsi na wadau wa kikanda, kuongeza ushiriki wa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kuongeza ukuaji wa soko la DSE.

Kwa upande wake, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Charles Shirima alisema ili kuwezesha ushiriki wa wananchi wengi mijini na vijijini katika uwekezaji wa masoko ya mitaji, mamlaka hiyo imehimiza matumizi ya mifumo bunifu katika uuzaji na ununuzi wa dhamana za masoko ya mitaji kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ikiwa ni pamoja na simu za mikononi na intaneti.

Alisema jitihada hizi zimewezesha kuanzishwa kwa mifumo kadhaa ikiwepo ya Sim Invest, Hisa Kiganjani, WekezaWHI na M-Wekeza ambayo inatumika kurahisisha upatikanaji wa huduma za masoko ya mitaji kwa wananchi wengi zaidi mijini na vijijini.

"Kwa mfano asilimia 24.33 ya mauzo ya hisa kwa mwaka 2024, yalipitia katika mfumo wa teknolojia ya habari yakiwa yameongezeka kutoka asilimia 4.84 mwaka 2023."

Awali, Afisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Peter Situmbeko alisema tangu kuanzishwa kwake, soko hilo limeendelea kuongezeka thamani ya mauzo ya hisa pamoja na hamasa kwa wawekezaji.

Alisema thamani ya mauzo ya hisa ilifikia shilingi bilioni 369.4 sawa na ongezeko la asilimia 246 ikilinganishwa na kipindi kama hichi mwaka jana.

"Kiasi cha hisa zilizouzwa zilifikia milioni 272 ambalo ni ongezelo la asilimia 108 ikilinganishwa na kipindi kama hichi mwaka jana, hatifungani za Serikali pamoja na makampuni binafsi zilifikia jumia ya mauzo ya zaidi ya TZS 3 trilioni katika kipindi kama hichi mwaka jana mauzo haya yalifikia TZS 1.9 trilioni"




# BOT YAPEWA TUZO MAALUMU KUCHANGIA UJENZI MAONESHO YA MADINI

Wakati msimu wa nane wa maadhimisho ya Maonesho ya Teknolojia ya Madini ukitamatika Septemba 28, 2025, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imetunukiwa tuzo maalumu.

Tuzo hiyo iliyokabidhiwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa katika ufunguzi rasmi wa maonesho hayo Jumanne September 23, 2025 mkoani Geita ni ya kutambua mchango wa BoT katika ujenzi wa miundombinu ya kudumu katika viwanja hivyo.

Awali, viwanja hivyo havikuwa na majengo ya kudumu kwa ajili ya washiriki hivyo kulazimika kutumia matenti katika maonesho hayo yanayokusanya watu kutoka nchi mbalimbali.

Akizungumzia mchango wa BoT na taasisi nyingine katika ujenzi wa miundombinu hiyo ya kudumu, mhe. Majaliwa alisema itaongeza thamani na tija ya maonesho hayo katika sekta mbalimbali.

"Katika hili niyapongeze mashirika, taasisi na kampuni zote zilizochangia ujenzi wa miundombinu hii, kwa sababu itayaongezea thamani maonesho haya, ambayo kwa sasa watu kutoka nchi mbalimbali wanashiriki,"alisema.

Pia, Mhe. Majaliwa aliongeza kuwa; "Kutokana na miundombinu hii ya kudumu, sasa wafanyabiashara wanaweza wakaendelea na biashara zao katika eneo hili bila kutegemea uwepo wa maonesho."

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Bw. Emmanuel Shigella akizungumza katika ufunguzi wa maonesho hayo, aliyashukuru makampuni, mashirika na taasisi zote zilizochangia ujenzi huku akitaja adha iliyowakumba kipindi cha nyuma kabla ya ujenzi huo.

"Mheshimiwa Waziri Mkuu, nichukue nafasi hii kuwashukuru wadau wetu waliochangia ujenzi huu. Miaka ya nyuma katika viwanja hivi ilikuwa ukifika wakati wa maonesho tunaumia kichwa gharama za kukodi matenti.

"Kwa sasa hivi tumelipunguza hilo, na ujenzi bado unaendelea tuna mpango wa kupata majengo haya uwanja mzima ili maonesho yetu yawe na hadhi ya kimataifa. Na mwaka huu tuna wageni kutoka nchi mbalimbali,"alisema na kuongeza Shigella.



Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, akimkabidhi tuzo maalum Meneja Idara ya Mawasiliano, Bi. Victoria Msina, kwa udhamini wa ujenzi wa miundombinu ya kudumu katika viwanja vya Dkt. Samia Suhulu Hassan mkoani Geita.

Awali, kabla ya maonesho hayo kufunguliwa Mhe. Majaliwa, alitembelea banda la Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ambapo alipokelewa na Meneja, Idara ya Mawasiliano Benki Kuu, Bi. Victoria Msina, alipewa maelezo kuhusu Mpango wa Benki Kuu wa Ununuzi wa Dhahabu ulioanza tarehe 1 Oktoba 2024.

Bi. Msina alisema; "Mpango huu umeleta mafanikio makubwa katika kuongeza hifadhi ya fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya Shilingi ya Tanzania. Hadi kufikia sasa, jumla ya tani 10 zimenunuliwa na BoT,"alisema.

Bi. Msina aliongeza kuwa mpango huo umefungua fursa kwa wachimbaji na wauzaji wa dhahabu nchini kuuza dhahabu zao moja kwa moja kwa Benki Kuu ya Tanzania kwa bei ya ushindani kulingana na soko la kimataifa.

# MWENENDO WA MFUMUKO WA BEI WA NDANI - SEPTEMBA 2025

## MFUMUKO WA BEI WA JUMLA

| Agosti, 2025 | September, 2025 |
|---|---|
| 3.4% | 3.4% |

Ulisalia kuwa asilimia 3.4 mwezi Septemba 2025, kiwango sawa na kilichorekodiwa mwezi Agosti 2025. Utulivu huu umetokana hasa na kupungua kwa bei za vyakula, kulikosaidia kufidia ongezeko la bei za bidhaa zisizo za chakula.

## MFUMUKO WA BEI WA BIDHAA ZA CHAKULA

| Agosti, 2025 | September, 2025 |
|---|---|
| 7.7% | 7.0% |

Ulipungua hadi asilimia 7.0 kutoka asilimia 7.7 mwezi uliopita. Hali hii imesababishwa na kupungua kwa bei za bidhaa muhimu za chakula kama vile mtama, mahindi, mihogo, viazi mviringo, ndizi, kuku, nyama ya ng'ombe, samaki wabichi na mafuta ya kupikia. Kupungua kwa bei hizi kunahusishwa na uzalishaji wa kutosha wa chakula nchini.

## MFUMUKO WA BEI WA BIDHAA ZISIZO ZA CHAKULA

| Agosti, 2025 | September, 2025 |
|---|---|
| 1.6% | 1.9% |

Uliongezeka hadi asilimia 1.9, ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwezi Agosti 2025. Ongezeko hili limechangiwa zaidi na kupanda kwa bei za pombe kali, sigara, vifaa vya ujenzi (hasa saruji), gesi ya kupikia, mkaa, samani, vitambaa vya nguo, na viatu vya wanaume.

## MFUMUKO WA BEI WA KUNDI LA NISHATI, MAFUTA NA HUDUMA

| Agosti, 2025 | September, 2025 |
|---|---|
| 2.6% | 3.7% |

Uliendelea kupanda na kufikia asilimia 3.7 mwezi Septemba 2025, kutoka asilimia 2.6 mwezi uliotangulia. Hali hii imetokana hasa na kupanda kwa bei za gesi ya kupikia na mkaa.

## MFUMUKO WA BEI USIOHUSISHA BEI ZA VYAKULA NA NISHATI

| Agosti, 2025 | September, 2025 |
|---|---|
| 2.0% | 2.2% |

Uliongezeka hadi asilimia 2.2 mwezi Septemba 2025, kutoka asilimia 2.0 mwezi Agosti 2025.

*Chanzo: Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS)*

# DKT. MPANGO: MAKUMBUSHO YA BOT NI NYENZO MUHIMU YA ELIMU KWA UMMA



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Makumbusho ya Benki Kuu ya Tanzania, uliyofanyika tarehe 30 Julai, 2025 katika ofisi za BOT jijini Dar es Salaam. Kutoka kushoto ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar, Dkt. Juma Malik Akil, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry Silaa (Mb), Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, Waziri wa Nchi, Ofisis ya Rais-Fedha na Mipango Zanzibar, Dkt. Saada Mkuya (Mb) na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Chande (Mb).

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango, ameipongeza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kuanzisha Makumbusho ya Benki Kuu ya Tanzania inayolenga kuelezea historia ya fedha nchini na ya Benki Kuu ya Tanzania pamoja mageuzi mbalimbali ya sekta ya fedha katika muktadha wa tulikotoka, tulipo na tunakoelekea.

Akizungumza baada ya kuzindua rasmi makumbusho hiyo Dkt. Mpango ameilezea kuwa ni nyenzo muhimu ya kuelimisha umma hususan vijana ili wapate uelewa wa historia na mageuzi mbalimbali yaliyofanyika katika sekta ya fedha.

"Hongereni kwa kazi kubwa na nzuri mlioifanya. Ninapowapongeza, nawaomba pia muwahamasishe vijana wetu waje kwenye makumbusho haya ili wapate picha halisi ya mageuzi yaliyofanyika nchini katika sekta ya fedha. Hii ni sehemu muhimu sana ya mafunzo," alisisitiza Dr. Mpango.

Katika hatua nyingine, Dkt. Mpango, ameipongeza Benki Kuu kwa kuanzisha Maktaba Mtandao akieleza kuwa ni hatua muhimu katika kuhamasisha vijana kupenda kujisomea.

"Kama tunasema asilimia kubwa ya watanzania wapo miaka 35 kurudi chini, maana yake tunahitaji taifa ambalo linasoma. Tuhamasishe vijana wetu kupenda kujisomea. Sasa kwa kuwa kuna huduma kama hizi ina maana mtu haitaji tena kutafuta nakala ngumu anaweza kuingia kwenye simu yake akasoma". Ameeleza.

Makumbusho hii huwa wazi siku za Jumatatu, Jumatano na Ijumaa kuanzia 3:00 Asubuhi hadi saa tisa Alasiri. Kwa wananchi wanaopenda kutemebelea wanaweza kuwasilisha maombi yao kupitia barua pepe botcommunications@bot.go.tz

Dr. Mpango alifanya uzinduzi wa Makumbusho ya BOT na Maktaba Mtandao, tarehe 30 Julai, 2025 katika ofisi za Benki Kuu jijini, Dar es Salaam.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango, akizindua Makataba Mtandao ya Benki Kuu ya Tanzania katika hafla iliyofanyika tarehe 30 Julai, 2025.



Meneja wa Idara ya Mawasiliano wa Benki Kuu ya Tanzania, Bi. Victoria Msina, akimwelezea Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango, maudhui mbalimbali ya Makumbusho ya BOT baada ya uzinduzi rasmi wa makumbusho hiyo.




# TISEZA YAZINDUA MAENEO MAALUM YA KIUCHUMI

Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA) ilizindua rasmi Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZs) tarehe 12 Agosti 2025 jijini Dar es Salaam, ikiwa na lengo la kuvutia uwekezaji mkubwa wa viwanda na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara na uwekezaji barani Afrika.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mhe. Prof. Kitila A. Mkumbo alisema tangu kuanzishwa kwa TISEZA, Serikali imeendelea kuimarisha uwekezaji katika SEZs kwa kuziunganisha na miradi mikubwa ya miundombinu kama vile Reli ya Kisasa (SGR), barabara kuu, bandari na viwanja vya ndege.

Prof. Mkumbo alitaja maeneo matano ya kimkakati yanayotangazwa kwa uwekezaji kuwa ni Nala SEZ (Hekta 607), Kwala SEZ (Hekta 40.5 – ekari 100), Buzwagi SEZ (Hekta 1,333), Bagamoyo Eco Maritime City – BEMC SEZ Awamu ya Kwanza (Hekta 151) na Benjamin William Mkapa SEZ (Upanuzi) yenye mita za mraba 13,000.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Dkt. Tausi Kida, alisema kuwa uzinduzi wa Kampeni ya Kitaifa ya Uhamasishaji Uwekezaji katika SEZs ni nyenzo muhimu ya kukuza uchumi kupitia ajira, mauzo ya nje, uhamisho wa teknolojia na ubunifu wa viwanda.

Dkt. Kida aliongeza kuwa kuunganisha SEZs na miundombinu mikubwa ya kimkakati kama SGR, bandari na viwanja vya ndege kutajenga msingi imara wa mageuzi ya kiuchumi yatakayogusa kila mkoa wa Tanzania.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TISEZA, Bw. Giread Teri, aliwataka wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa kutoka nje ya nchi kuchangamkia fursa za kuanzisha viwanda nchini, akibainisha kuwa serikali inatoa maeneo bure kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.

"Waje wazalishe kwa soko la ndani, soko la Afrika Mashariki na hata kuuza nje ya bara. Vivutio vingi vimetolewa na serikali na leo tumeyazindua rasmi," alisema Bw. Teri.

Maeneo haya ya kimkakati yanatarajiwa kuleta manufaa makubwa kwa Taifa ikiwemo ajira kwa maelfu ya vijana, kuongeza mauzo ya nje, kupunguza uagizaji bidhaa na kuhamisha teknolojia mpya za viwanda nchini.

# TANZANIA, BURUNDI ZASAINI UJENZI SGR KILOMITA 300, FAIDA ZATAJWA



Safari ya siku nne kwa lori la mizigo inaenda kuwa ya saa 20, huku ile ya takribani siku mbili kwa kutumia basi itakuwa ya siku moja bila uchovu kwa abiria.

Kauli hiyo inaenda kuwa uhalisia punde tu utakapokamilika ujenzi wa Reli ya Kisasa ya Umeme (SGR) kutoka Dar es Salaam nchini Tanzania hadi Bujumbura nchini Burundi, ambapo jiwe la msingi la mradi huo wa kilomita 300 tayari limewekwa.

Akizungumza wakati wa uwekaji wa jiwe hilo la msingi kwa kipande cha Uvinza mkoani Kigoma hadi Musongati nchini Burundi Agosti 16, 2025 Waziri Mkuu wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa alisema; "Reli ikikamilika itafungua fursa kwa wananchi wetu ambao wataweza kutoka hapa hadi Dar es Salaam ndani ya siku moja. Hata kwenye usafirishaji wa mizigo, hivi sasa, lori linatumia saa 96 (siku nne) kutoka Dar hadi Bujumbura lakini baada ya kukamilisha ujenzi, usafirishaji wa mizigo kwa kutumia treni utatumia saa 20 tu."

Jiwe la msingi la mradi huo lilizinduliwa na Rais wa Burundi, Mhe. Evarist Ndayishimiye pamoja na Mhe. Majaliwa kwa upande wa Tanzania akimuwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa upande wake, Rais Ndayishimiye alisema kuanza kwa ujenzi wa reli hiyo kutatibu shauku ya muda mrefu ya nchi hiyo kuwa na usafiri wa reli.

"Leo ni siku ya furaha sana kwetu. Tumepata jawabu la tangu enzi na enzi. Mwaka 1921, mradi huu ulianzishwa na Wabelgiji kisha wakaja Wajerumani lakini wakashindwa. Leo hii Tanzania na Burundi tumeweza," alisema.

**Manufaa ya kiuchumi**

Akizungumzia namna reli hiyo itakavyochagiza uchumi wa Burundi na Tanzania, Rais Ndayishimiye alisema nchi yake ina madini mengi lakini ilikuwa ngumu kwa wawekezaji kuwekeza.
"Wengi walivutiwa na wakataka kuwekeza mara moja, lakini wakaniuliza, tukianza kuchimba madini ya nikeli, tutayasafirishaje?"

"Hiyo changamoto ilitufanya tubungue bongo zetu na kutafuta suluhisho. Tunaishukuru sana Serikali ya Tanzania kwa kukubali kuungana nasi ili tuanze mradi huu muhimu. Tukitoka hapa, tunataka reli iunganishe hadi Kindu, Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC). Na baada ya hapo, ifike Afrika Magharibi kwenye ufukwe wa Bahari ya Atlantiki kwani tunaamini njia hiyo itaharakisha kuleta maendeleo,"alisema na kuongeza Rais Ndayishimiye.

Kwa mujibu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), katika kilomita 300 zitakazojengwa baina ya nchi hizo mbili, kilomita 240 ni njia kuu na kilomita 60 ni njia za kupishania pamoja na stesheni za mizigo na abiria.

"Kwa upande wa Tanzania mradi huo utakuwa na kipande chenye urefu wa kilomita 190 wakati kipande cha Musongati (Burundi) kitakuwa na urefu wa kilomita 110,"imeeleza taarifa ya TRC katika tovuti yake.

Mradi huo unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa gharama ya dola za Marekani bilioni 2.54 sawa na fedha za Tanzania shilingi trilioni 5.1 utakuwa ndiyo reli ya kwanza inayounganisha nchi na nchi katika ukanda wa Afrika Mashariki na unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miaka sita.

**Faida za reli hiyo**

Kwa mujibu wa tovuti ya TRC katika taarifa yake iliyoichapisha kuhusu mradi huo imesema; "Kukamilika kwa ujenzi wa reli hiyo kutasaidia kuunganisha masoko na kuendeleza biashara baina ya Tanzania na Burundi pia kunatarajiwa kuokoa muda wa usafiri na usafirishaji kati ya Dar es Salaam na Burundi."

Akizungumzia umuhimu wa kukamilika kwa mradi huo, Waziri wa Uchukuzi wa Tanzania, Profesa Makame Mbarawa alisema mbali na kuziunganisha nchi hizo mbili, pia kupunguza gharama za usafirishaji wa mizigo.

"Hivi sasa, kontena moja la futi 20 linasafirishwa kwa gharama ya dola za Marekani 3,800 lakini reli hiyo itakapokamilika, gharama itashuka hadi dola za Marekani 2,000.

"Hivi sasa, mzigo unaosafirishwa kwa lori moja ni tani 30, lakini reli ikianza kazi, tutaweza kusafirisha tani 3,000 kwa wakati mmoja," alisema na kuongeza Profesa Mbarawa.

Reli hiyo itakuwa kichocheo cha maendeleo ya viwanda, kilimo, sekta ya madini na sekta nyingine za uzalishaji kwa kutoa huduma ya usafiri wa uhakika
Pia, Profesa Mbarawa alibainisha kuwa utekelezaji wa mradi huo unaenda sambamba na Ajenda 63 ya Umoja wa Afrika (AU) ambayo inataka Bara la Afrika liunganishwe kwa mtandao wa reli ya kisasa.

Rais Ndayishimiye alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufikia hatua kubwa za maendeleo na kuchagiza biashara ya nchi hizo mbili.



# MPANGO WA UNAFUU WA GHARAMA ZA SIMU AFRIKA MASHARIKI WAZAA MATUNDA

Gharama za maongezi kwa simu kutoka Tanzania kwenda nchi nyingine Afrika Mashariki zilishuka kwa asilimia 61 kati ya Aprili na Juni 2025 kufuatia utekelezaji wa makubaliano ya pamoja kupunguza gharama za simu kwa watumiaji wanaotembelea mojawapo ya nchi hizo, taarifa zimethibitisha.

Ripoti ya Hali ya mawasiliano Tanzania katika robo mwaka ya Aprili hadi Juni mwaka huu inaonesha kuwa wastani wa gharama za siku kwenda nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zilipungua kutoka TZS 627.80 kwa dakika Machi hadi TZS 247.52 Juni mwaka huu.

Ripoti hiyo, iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Dkt Jabiri Bakari inaeleza kuwa dakika za maongezi ya simu kutoka Tanzania kwenda nchi nyingine EAC zimeongezeka kutoka 9,097,165 robo mwaka ya Aprili-Juni 2021 hadi 156,913,941 Aprili-Juni 2025.

Kwa simu za humu nchini, wastani wa bei za kupiga simu (bila kifurushi) haujabadilika tangu Juni mwaka jana. Umebakia shilingi 26 kwa simu kwenye mtandao wa mtumiaji (on-net) na TZS 28 kwenda mtandao mwingine (off-net).

Meseji (SMS) za ndani zinatozwa TZS 7.80 na za kwenda nje TZS 189.60 kwenye mitandao yote. Bei za data zimebakia TZS 9.35 kwa megabaiti (MB).

MB ni kipimo cha ukubwa wa data kwenye matumizi ya kompyuta, ambamo kila herufi, namba, alama ni baiti moja. Zikiwa 100 ni kilobaiti (KB) na elfu ni megabaiti (MB).

Uchambuzi wa ripoti ya TCRA unabainisha kuwa wastani wa gharama za kupiga simu unatokana na gharama ndogo za mtoa huduma mmoja anayetoza chini ya wastani kwa kiasi kikubwa. Halotel wanatoza TZS 10 kwa maongezi kwenye mtandao wao, TZS 20 kwenda mitandao mingine na shilingi tano (5) kwa SMS.

Airtel, Yas, TTCL na Vodacom wanatoza TZS 30 kwa maongezi ndani na nje ya mitandao na shilingi nane (8) kwa meseji.

Gharama za kupiga simu bila kifurushi zilipungua kwa asilimia 21 kati ya Juni 2021 na Juni mwaka huu – kutoka TZS 34 kwa dakika ndani na nje ya mitandao. Bei za SMS za ndani zimepungua kwa asilimia 67 – kutoka TZS 13 hadi zinazotozwa sasa.

Kwa upande wa vifurushi, gharama za simu ndani ya mtandao zimebakia TZS 4.80 tangu Septemba 2024 wakati nje ya mtandao zimeshuka kutoka TZS 6.07 kwa dakika machi 2025 hadi 5.96 Juni mwaka huu. Vifurushi vya data vinatozwa TZS 2.12 kwa MB na SMS za ndani TZS 2.12.

Gharama za vifurushi vya maongezi zilishuka kwa asilimia 71 kati ya Juni 2021 na Juni mwaka huu – kutoka wastani TZS 8.3 kwa dakika kwenye mitandaoi yote hadi zinazotozwa sasa. Bei za vifurushi vya data zilikuwa TZS 1.61 kwa MB mwaka 2021, zikaongezeka hadi TZS 2.17 na kubakia TZS 2.12 kuanzia Machi mwaka huu.

Ripoti inasema wateja wa mitandao ya simu za mkkononi walitumia dakika bilioni 43.3 kwenmye robi mwaka ya Aprili hadi Juni mwaka huu, kutoka bilioni 40.6 billion robo mwaka iliyoishia Machi mwaka huu.

Wakati huo huo, simu zenye uwezo mkubwa, maarufu kama simu janja, zimeenea kwa asilimia 37 miongoni mwa watu. Hii inawezesha watumiaji wengi kutumia huduma zinazotokana na teknolojia za kisasa na za uzao wa mbele wa mawasiliano kupitia vifaa vya mkononi.

Taarifa hiyo imesema ueneaji wa teknolojia za uzao wa tatu (3G) na wa nne (4G) uliongezeka kwa kati ya asilimia 11 na tano kati ya Juni 2024 na Juni mwaka huu. Kuenea kijiografia nchini kuliongezeka kwa asilimia 8.7 Kati ya Juni 2024 na Juni 2025.

Uzao wa tatu umeenea miongoni mwa watu asilimia 93.4 ya watu, kutoka 89 na uzao wa nne asilimia 92 kutoka 83 kipindi hicho. Kuenea 3G kijiografia ni asilimia 75, kutoka 73 na 4G asilimia 75, kutoka 69.

Uzao wa 5G ulienea kwa kwa asilimia 5.9 miongoni kwa watu kufikia Juni 2025 kutoka asilimia 2 Juni mwaka jana na asilimia 3.6 ya watu Machi mwaka huu. Teknolojia hiyo imefika asilimia 26 ya eneo la Tanzania, kutoka asilimia 15 Juni 2024 na 23 Machi mwaka huu.

# TIRA INAVYOTEKELEZA SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE KWA MAENDELEO YA TAIFA

Kupitia Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote (UHI) namba 13 ya mwaka 2023, Tanzania imepiga hatua kubwa kuelekea kuhakikisha huduma bora za afya zinapatikana kwa kila raia.

Sheria hii iliyoanza kutumika rasmi Agosti 16, 2024, inalenga kuimarisha afya ya Watanzania kwa kupunguza mzigo wa gharama za matibabu, hivyo kuboresha hali ya maisha ya wananchi wote bila kujali kipato au mazingira yao.

Sheria hii ni mojawapo ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ametilia mkazo umuhimu wa kuwa na mfumo wa afya wenye kuwajumuisha Watanzania wote.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), ikiwa msimamizi wa sheria hii, inawajibika kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Katika kuhakikisha lengo hili linatimia, kanuni za utekelezaji wa sheria hii zilizoainishwa kupitia tangazo la serikali Na. 809 la Septemba 13, 2024 zinaeleza kwa undani jinsi watoa huduma za bima na wanachama watakavyopaswa kushirikiana ili kuhakikisha kila mmoja anapata huduma bora.

**Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, sheria inatoa haki ya msingi kwa kila Mtanzania kuwa na bima ya afya. Hii inahusisha raia wote wa Tanzania na wageni wanaoishi nchini, bila kujali kama wanatoka sekta rasmi au isiyo rasmi. Katika kutekeleza hilo, TIRA imekuwa na jukumu la kusimamia skimu zote za bima ya afya, kuhakikisha watoa huduma wanafuata taratibu sahihi za usajili wa wanachama, na pia kufuatilia utekelezaji wa huduma zinazotolewa.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 7(2), TIRA imepewa mamlaka ya kuhakikisha kuwa watoa huduma wa bima ya afya wanatoa huduma bora na za haki kwa wanachama waliopo kwenye skimu zao. Kanuni zinaeleza wazi kuwa skimu za bima lazima ziwasajili wanachama kwa uwazi na kuhakikisha michango inawasilishwa kwa wakati.

**Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote za Mwaka 2024**

Sheria hii imeambatana na Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote za mwaka 2024, ambazo zinaelekeza namna skimu za bima zinavyopaswa kutekelezwa. Kanuni hizo zimegawanyika katika sehemu Nane ambazo ni Masharti ya utangulizi, usajili wa skimu za bima ya afya, utambuzi na usajili wa watu wasio na uwezo, usimamizi na udhibiti wa huduma za bima ya afya, usajili wa wanachama, vitita vya mafao, utaratibu wa malipo kwa vituo vya kutolea huduma za afya na masharti ya jumla.

**Jinsi Bima ya Afya kwa Wote Inavyofanya Kazi kwa Mujibu wa Kanuni**

Kwa mujibu wa kanuni za Bima ya Afya kwa Wote, skimu zote za bima zinapaswa kufuata taratibu zifuatazo ili kuhakikisha utekelezaji wake unafanikiwa:



Usajili wa Skimu za Bima ya Afya: Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 (1), Mtu yeyote anayekusudia kutoa huduma za bima ya afya kama skimu ya bima ya afya binafsi atawasilisha kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania maombi ya usajili, hivyo skimu zote za bima ya afya zinapaswa kusajiliwa na TIRA.

Utambuzi na usajili wa watu wasio na uwezo: Kifungu cha 13 (1) kinaelekeza kuwa watu wasio na uwezo watagharamiwa na serikali kupitia mfuko maalum ambapo utambuzi wa watu hao utasimamiwa na Serikali. Aidha kipengele cha 16 (1) kinaeleza kuwa watu waliotambuliwa na kuingizwa katika kanzidata ya watu wasio na uwezo watapata huduma za afya kwa utaratibu wa bima ya afya chini ya skimu ya bima ya afya ya umma kwa kugharimiwa na Serikali kuptia Mfuko.

Usimamizi na udhibiti wa huduma za bima ya afya: Kifungu cha 17 (1) TIRA itasimamia na kudhibiti skimu za bima ya afya kwa kufuatilia huduma zinazotolewa ili kuhakikisha kuwa wanachama wanapata huduma kwa ubora na kwa wakati. Aidha kwa mujibu wa kifungu cha 19 (1) TIRA itafanya ukaguzi wa skimu za bima ya afya kila mwaka kwa kuzingatia taratibu na miongozo ya ukaguzi iliyowekwa na Mamlaka.

Usajili wa wanachama katika skimu za bima ya afya: Kipengele cha 20 (1) kinaelekeza kwamba kila raia au mkazi katika sekta rasmi na isiyo rasmi atakuwa na haki ya kusajiliwa katika skimu ya bima ya afya kwa utaratibu utakaowekwa na skimu ya bima ya afya kupitia miongozo yake ambayo itaidhinishwa TIRA.

Aidha kipengele cha 22 (1) kinaeleza kwamba skimu ya bima ya afya inaweza kuweka muda wa kusubiri wa mwanachama na mnufaika aliyesajiliwa katika skimu hiyo kabla ya kuanza kunufaika na huduma za bima ya afya. Isipokuwa kwamba, muda huo wa kusubiria hautazidi siku thelathini tangu tarehe ya mwanachama au mnufaika kusajiliwa.

Pia kipengele cha 23 (1) kinaeleza bayana kuhusiana na mwajiriwa katika sekata rasmi binafsi kuingia mkataba na skimu ya bima ya afya moja kwa lengo la kuwasajili waajiwa wake ili kupata kitika cha mafao cha huduma muhimu au kitika cha huduma za ziada.

# TIRA INAVYOTEKELEZA SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE KWA MAENDELEO YA TAIFA




Kipengele cha 23 (2) skimu ya bima ya afya ya umma inaweza kuingia mkataba na mwajiri katika sekata ya umma au binafsi kwa masharti yatakayowekwa kwa mujibu wa sheria inayosimamia skimu ya bima ya afya ya umma.

Vilevile Kifungu cha 27 (1) kinatoa notisi ya kituo cha kutolea huduma ya afya kinachosudia kusitisha utoaji wa huduma kwa wanachama na wanufaika wa skimu ya bima ya afya kutoa notisi hiyo ya maandishi ya muda wa siku Tisini kwa skimu na nakala kwa TIRA ikibainisha kusudio la kusitisha huduma na sababu ya kusudio hilo.

Vitita vya mafao: Sehemu ya sita ya Kanuni imeeleza kwamba kutakuwa na aina mbili ya vitita vya mafao ambazo ni; kitita cha mafao ya huduma muhimu na kitita cha huduma za ziada. Kifungu cha 30 (1) kinaelezea kitita cha mafao ya huduma muhimu kama haki ya mwanachama au mnufaika kupata huduma zifuatazo; uandikishaji na kumuona daktari, vipimo vya uchunguzi tiba vya maabara, radiolojia na mionzi, huduma za kulazwa, matibabu ya macho, kinywa na meno, huduma ya kujifungua na huduma ya upasuaji. Kifungu cha 35 kinaeleza madhumuni ya uanzishwaji wa kitika cha huduma za ziada ambapo TIRA itaandaa muongozo wa utoaji wa kitita hicho ambacho kimsingi kitita kitatoa huduma za ziada na kitaonesha viwango vya uchangiaji kwa kuzingatia tathmini ya uhai na uendelevu wa skimu ya bima.

Utaratibu wa malipo kwa vituo vya kutolea huduma za afya: Kifungu cha 36 (1) kinaeleza kuwa kituo cha kutolea huduma za afya kuwasilisha kwa skimu ya bima ya afya madai ya huduma zilizotolewa kwa mwanachama au mnufaika ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kukamilika kwa huduma ya matibabu. Kwa mujibu wa kifungu cha 36 (2) ni kosa kwa kituo cha huduma za afya kuwasilisha madai kwa skimu ya bima ya afya bila kutumia miongozo ya skimu za bima ya afya iliyoidhinishwa na TIRA.

Masharti ya jumla: Baadhi ya masharti ya jumla yanayotajwa kwenye kanuni hizi ni pamoja na hatua ambazo TIRA in aweza kuchukua kwa skimu ya bima ya afya ambayo imekiuka kanuni na sheria za bima ya afya ambazo ni pamoja na kutozwa kwa mujibu wa masharti ya sheria na kanuni za bima ya afya kwa wote au kufutiwa usajili.

**Hatua za Utekelezaji na Mchango wa TIRA**

Katika kuhakikisha utekelezaji wa sheria hii unakuwa wa ufanisi, TIRA imechukua hatua mbalimbali za kuhimiza wananchi kujiunga na skimu za bima. Hivi karibuni, TIRA imezindua mpango wa kutoa bima za afya kwa Watanzania 10,000, kwa kushirikiana na viongozi wa dini na taasisi mbalimbali. Mpango huu ulianza na utoaji wa kadi za bima 1,093 kwa Waziri Mkuu Mhe. Kassimu Majaliwa wakati wa Baraza la Maulid lililofanyika mkoani Geita.

Bima hizi zimepatikana kutokana na juhudi za kampuni za Assemble (500 kadi) na Strategis (593 kadi), ambapo wanufaika wataweza kupata matibabu kwa mwaka mzima kwenye hospitali zilizosajiliwa na kampuni hizo. Zoezi la kugawa bima za afya lililoanzishwa na Mufti wa Tanzania Dkt. Abubakar Zuber bin Ally, kwa kushirikiana na Kamishna wa Bima Dkt. Baghayo Saqware, ni sehemu ya kuhakikisha malengo ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote yanatimia.

**Umuhimu wa Bima ya Afya kwa Wote**

Bima ya afya kwa wote ni fursa muhimu katika kuhakikisha kuwa huduma za afya zinapatikana kwa kila mmoja kwa gharama nafuu. Kifungu cha 6(2) kinatoa haki kwa kila Mtanzania kuwa na bima ya afya ili kuhakikisha huduma za afya zinapatikana bila vikwazo vya kifedha. Hii inaondoa mzigo mkubwa kwa familia nyingi ambazo mara nyingi zimeshindwa kumudu gharama za matibabu.

Kupitia sheria hii, Watanzania wote watakuwa na uwezo wa kupata huduma za matibabu bila kulipa gharama kubwa, hali inayosaidia kuongeza usalama wa afya na ustawi wa kijamii. Wanachama wa skimu za bima ya afya wanapata huduma za matibabu kwa mwaka mzima, kwenye hospitali zote zilizo kwenye mtandao wa bima yao, kama inavyoelekezwa na Kifungu cha 10(4).

Bima ya Afya kwa Wote ni mabadiliko makubwa katika sekta ya afya nchini Tanzania, yanayohakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora za afya kwa gharama nafuu. TIRA, kama msimamizi wa utekelezaji wa sheria hii, inafanya kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa sheria inatekelezwa kikamilifu, huku ikihimiza usawa wa upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote.

Kupitia mradi wa bima za afya kwa Watanzania 10,000, TIRA imeonyesha kwa vitendo jinsi bima ya afya inaweza kuboresha maisha ya wananchi. "Afya ni Uhai", na kwa kupitia Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Tanzania inachukua hatua kubwa kuelekea kuwa na taifa lenye afya bora na maendeleo endelevu.

# NAFASI YA MASOKO YA MITAJI KUELEKEA UCHUMI SHINDANI NA JUMUISHI




Dira 2050 imeweka malengo ya kimageuzi ya kimaendeleo ya kuwa na Taifa lenye uchumi imara, jumuishi, na shindani ifikapo mwaka 2050. Dira inatoa angalizo kuwa ili kufikiwa kwa malengo hayo kunahitaji pamoja na masuala mengine, kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji ikijumuisha ujenzi wa miundombinu ya kisasa, masuala ambayo yatahitaji mifumo madhubuti ya upatikanaji wa rasilimali fedha.

Miongoni mwa utatuzi wa changamoto hizo ni pamoja na kutumia suluhu inayoletwa na mfumo wa masoko ya mitaji. Mfumo huu unawezesha upatikanaji wa rasilimali fedha za muda mrefu kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za umma na binafsi.

Masoko ya mitaji ni mfumo wa kifedha unaowezesha upatikanaji wa fedha za muda mrefu kwa njia ya kuuza kwa umma dhamana kama vile hisa za kampuni, hatifungani za serikali, hatifungani za kampuni na vipande vya mipango ya uwekezaji wa pamoja.

Bidhaa zinazopatikana katika masoko ya mitaji zinatoa fursa kwa Kampuni, Taasisi na Serikali kukusanya mtaji na wakati huohuo kutoa fursa kwa wananchi kujipatia kipato kwa kuwekeza akiba zao. Kwa njia hiyo, masoko ya mitaji yanawezesha kutekelezwa kwa azma ya ujenzi wa uchumi jumuishi kama ilivyoainishwa katika Dira 2050. Masoko ya mitaji husimamiwa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA).

### Kuongezeka kwa bidhaa bunifu katika masoko ya mitaji

Ugharamiaji wa shughuli za maendeleo unategemea vyanzo mbalimbali vya mapato, ikiwemo masoko ya mitaji ambayo yanatoa bidhaa zilizoandaliwa kwa lengo mahsusi la kuwapatia wananchi fursa ya kuwekeza fedha zao na kwa njia hiyo kufanikisha upatikanaji wa mitaji inayoweza kuendeleza miradi na hivyo kuchochea uchumi.

Aidha, masoko ya mitaji yanatoa njia mbadala kwa taasisi za serikali kuweza kupata fedha za kugharamia miradi ya maendeleo bila ya kupanga foleni ya kupatiwa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Njia hii inawezesha miradi ya taasisi hizo kutekelezwa kwa wakati na wakati huohuo kupunguza mzigo wa Mfuko Mkuu wa Serikali, kwa kuelekeza fedha za Mfuko huo kwenye huduma zingine za kijamii.

Kwa kutambua nafasi ya masoko ya mitaji katika kuwezesha maendeleo ya kiuchumi nchini, CMSA inatekeleza mikakati ya kupanua wigo wa bidhaa za masoko ya mitaji ili kukidhi mahitaji ya fedha za muda mrefu kwa maendeleo ya Uchumi.

Hivyo, CMSA imekuwa mstari wa mbele katika kujenga mazingira wezeshi kwa maendeleo ya masoko kupitia kuongeza bidhaa mpya na bunifu zinazovutia wawekezaji wa ndani na wa kimataifa. Aidha, CMSA imehamasisha matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma ili kuwafikia wananchi wengi, mijini na vijijini na hivyo kuongeza ujumuishaji wa wananchi katika mfumo rasmi wa fedha, hususan masoko ya mitaji.

Katika miaka ya hivi karibuni, CMSA imetoa idhini kwa bidhaa mbalimbali bunifu ambazo kwa pamoja zinaongeza wigo wa bidhaa, hivyo kutoa fursa pana kwa wawekezaji wenye malengo mbalimbali. Baadhi ya bidhaa hizo ni pamoja na hatifungani endelevu yaani hatifungani za kijani (green bonds); hatifungani za kijamii (social bonds); hatifungani zinazozingatia misingi ya

# NAFASI YA MASOKO YA MITAJI KUELEKEA UCHUMI SHINDANI NA JUMUISHI

kimaadili (Ethical Finance); na hatifungani zinayotolewa katika fedha mbalimbali (Multicurrency bonds).
Sambamba na hayo, Mamlaka imeidhinisha Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja unaowezesha wawekezaji kuwekeza kwa fedha za kigeni. Bidhaa hizi zinaimarisha nafasi ya masoko ya mitaji ya Tanzania kwenye ramani ya masoko ya mitaji ya kimataifa hivyo kuvutia wawekezaji wa ndani na nje.

Dhana ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi
Upatikanaji wa vyanzo mseto vya fedha ni hatua muhimu katika kufikia malengo ya maendeleo. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ni dhana inayowezesha ushirikiano wa kimkakati ambao utarahisisha upatikanaji wa rasilimali fedha zitakazotumika kwa maslahi mapana ya Taifa.

Masoko ya Mitaji ni jukwaa muhimu la kufanikisha dhana hii ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi. Uzingatiaji wa uwazi, ukwasi, na mitaji endelevu unafanya mifumo hii kuwa kiungo kikubwa cha kufanikisha dhana ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi.
Jukwaa hili linatoa fursa endelevu za ushirikiano kati ya Sekta Binafsi na Taasisi za Umma katika kufanikisha miradi mbalimbali ya maendeleo. Mfano mzuri ni Hatifungani ya Miundombinu ya Samia ambayo ilitolewa kwa ubia kati ya Benki ya CRDB na Wakala wa bara bara nchini (TARURA).

Hatifungani hii, iliweza kukusanya kiasi cha TZS 323.1 bilioni ikilinganishwa na lengo la kukusanya TZS 150 bilioni sawa na mafanikio ya asimilia 215.4. Fedha hizi zinatumika kufadhili miradi muhimu ya miundombinu nchini Tanzania, hasa ujenzi wa barabara chini ya Wakala wa Barabara Vijijini na Vilevile hatifungani ya Kijani ya Miundombinu ya Maji (Tanga Water Infrastructure Green Bond) iliyotolewa na Manispaa ya Tanga kupitia Taasisi yam aji Tanga (Tanga Uwasa) iliweza kukusanya kiasi cha TZS 54.72 bilioni sawa na mafanikio ya asilimia 103 ikilinganishwa na lengo la kukusanya TZS 53.12 bilioni.

Fedha hizi zinatumika kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya maji kwa wananchi wa Jiji la Tanga.

Bidhaa nyingine bunifu ni utoaji wa Hatifungani ya kijani, inayoitwa "CRDB Kijani Bond", ambapo kiasi cha TZS 171.83 bilioni kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 430, ikiwa ni toleo la kwanza la Hatifungani yenye thamani ya TZS 780 bilioni iliyoidhinishwa na CMSA. Fedha zilizopatikana zinatumika kutekeleza biashara na miradi rafiki kwa mazingira.

Mfano mwingine ni kutoka Soko la Hisa la Nairobi (Nairobi Securities Exchange - NSE). Katika miaka ya hivi karibuni, Kenya imeshuhudia ongezeko la uwekezaji wa kigeni kupitia masoko ya mitaji, hususan katika sekta za benki, simu, na nishati. Mfano mzuri ni kampuni ya simu ya Safaricom, ambayo iliorodheshwa kwenye NSE na kuweza kupanua biashara yake kwa kutumia fedha zilizopatikana kupitia masoko ya mitaji.

Halikadhalika, Afrika Kusini inayotumia masoko ya mitaji kukuza sekta ya viwanda, hasa katika kuboresha uzalishaji wa bidhaa za ndani na kuongeza ajira kwa wananchi wake. Mfano mzuri ni kampuni ya Sasol Limited ambayo ni kampuni kubwa ya uzalishaji wa nishati na kemikali. Kampuni hii ilitumia masoko ya mitaji kupata fedha za kuwekeza katika utafiti na maendeleo (R&D) ili kuboresha teknolojia za uzalishaji wa nishati na kemikali.

Fedha hizi pia ziliwekezwa katika ujenzi wa viwanda vipya, jambo ambalo limeongeza uzalishaji na kuleta ajira kwa maelfu ya watu.
India imetumia masoko ya mitaji kutoa mikopo kwa sekta ya kilimo. Mfano mmoja ni kampuni ya National Bank for Agriculture and Rural Development (NABARD) ambayo imekuwa ikitumia masoko ya mitaji kwa kutoa hatifungani na kupata fedha za kuwekeza katika miradi ya kilimo.
Masoko ya mitaji yana mchango mkubwa katika utekelezaji wa Dira ya Taifa kwa kutoa njia ya kukusanya fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kuvutia uwekezaji wa kigeni, kukuza sekta mbalimbali za uchumi, na kuongeza ajira. Mifano ya Tanzania, Kenya, Afrika Kusini na India, inaonyesha wazi jinsi masoko ya mitaji yanavyoweza kutumika kama chombo muhimu cha kufanikisha malengo ya maendeleo ya taifa, hasa katika sekta za miundombinu, kilimo, viwanda, teknolojia, na fedha.



Mgeni rasmi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango (wa tatu kulia) akipokea hati ya idhini ya uzinduzi wa Hatifungani ya Miundombinu ya Samia (Samia Infrastructure Bond) kutoka kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, CPA. Nicodemus Mkama (wa pili kushoto) katika sherehe rasmi ya kuidhinisha Hatifungani ya Miundombinu ya Samia.




Katika picha ya pamoja, Wadau wa Masoko ya Mitaji wakiwa katika hafla ya uorodheshwaji wa hatifungani ya Kijani ya Miundombinu ya maji (Tanga Uwasa Water Green Bond).




Mh. Dkt. Saada Mkuya Salim (Mb.), Waziri wa Fedha – Zanzibar akipiga kengele kuashiria kuorodheshwa rasmi kwa Zanzibar Quasi-Sovereign Sukuk katika Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE) ulioshuhudiwa na menejimenti ya DSE na CMSA.



Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, CPA. Nicodemus Mkama akizungumza wakati wa ufunguzi wa mfuko wa uwekezaji wa pamoja wa iDollar unaosimamiwa na Kampuni ya itrust Finance Ltd.

# DIB YAANDIKA HISTORIA: YAMPATA MKURUGENZI MKUU WA KWANZA

Bodi ya Bima ya Amana (DIB) imepiga hatua kubwa kuelekea kujitegemea kufuatia kuteuliwa kwa Mkurugenzi Mkuu wake wa kwanza, Bw. Isack Nikodem Kihwili.

Uteuzi huo wa kipindi cha miaka mitano kuanzia Agosti 1, 2025, umefanywa na Bodi ya Wakurugenzi wa DIB na kutangazwa na Mwenyekiti wa Bodi hiyo na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba.

Akitangaza uteuzi huo, Gavana Tutuba alisema DIB iko katika hatua za mwisho za kujitoa Benki Kuu ya Tanzania na kuwa taasisi inayojitegemea na kwamba tayari Serikali imeidhinisha muundo mpya wa taasisi hiyo.

"Kama sehemu ya utekelezaji wa muundo mpya ulioidhinishwa, Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Bima ya Amana imemteua Bw. Isack Nikodem Kihwili kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Bima ya Amana kwa kipindi cha miaka mitano ijayo," alisema Gavana Tutuba katika tangazo lake.

Hadi uteuzi huo mpya, Bw. Kihwili alikuwa ni Mkurugenzi wa DIB, ambayo kwa mujibu wa utaratibu wa awali ilikuwa moja ya kurugenzi ndani ya Benki Kuu ya Tanzania.

Bodi ya Bima ya Amana ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Fedha ya mwaka 1991 na kuanza kufanya kazi mwaka 1994 kama idara ndani ya Benki Kuu ya Tanzania, ikiwa na Bodi yake ya Wakurugenzi chini ya uenyekiti wa Gavana wa Benki ya Tanzania.

DIB inaendelea kufanya shughuli zake chini ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kwamba sasa iko katika hatua za mwisho kuwa taasisi inayojitegemea kama ilivyo kwa taasisi kama hizi duniani kote.

Majukumu ya Bodi ya Bima ya Amana ni kukinga amana za wateja katika benki na taasisi za fedha na kulipa fidia endapo benki au taasisi ya fedha itaanguka au kufilisika; kutathmini na kukusanya michango kutoka benki na taasisi za fedha zinazopokea amana, na kusimamia Mfuko wa Bima ya Amana.

DIB pia ina wajibu wa kufanya ufilisi wa benki au taasisi ya fedha iliyoshindwa kuendelea na biashara ya huduma za kibenki au iliyofilisika endapo ikiteuliwa na Benki Kuu ya Tanzania kama mfilisi.

Aidha, kuanzia Julai 2025, DIB imeongezewa jukumu la kushiriki katika kupunguza hasara kwa benki au taasisi ya fedha inayotetereka ili irejee katika uendeshaji wa kawaida.



Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Bima ya Amana (DIB)

## BW. ISACK NIKODEM KIHWILI

# BOT, WADAU WAJADILI UWEZESHAJI BIASHARA NA UBUNIFU WA KIFEDHA




Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Dkt. Yamungu Kayandabila (katikati), pamoja na viongozi wa kampuni ya Viaservice Group baada ya ziara katika ofisi za Benki Kuu jijini Dar es Salaam tarehe 25 Agosti 2025. Kutoka kulia ni Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki, Bw. John Mathenge; Mjumbe wa Bodi ya Viaservice – Asiye Mtendaji,Bw. Abdulsamad Abdulrahim, Mkurugenzi Mtendaji wa Uwezeshaji Biashara, Bw. Morgan Lepinoy na Afisa Mkuu wa Fedha wa Kanda, Bi. Veronica Mhenga.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imekutana na kujadiliana na miongoni mwa wadau wa sekta ya fedha kuhusu mustakabali wa uwezeshaji biashara na ubunifu wa kifedha.

Mazungumzo hayo yenye tija katika sekta ya fedha yamefanyika Agosti 25, 2025 na Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dkt. Yamungu Kayandabila, na uongozi wa juu wa kampuni ya Viaservice Group, katika ofisi za Benki Kuu jijini Dar es Salaam.

Mazungumzo hayo yalijikita katika mustakabali wa uwezeshaji biashara na ubunifu wa kifedha katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Pamoja na hayo, pande zote mbili zilijadili Viaservice Container Solution (VCS), jukwaa la teknolojia ya kifedha linaloshughulikia changamoto za muda mrefu katika amana za makontena, ambalo linaweza kuondoa zaidi ya Dola bilioni 1.5 za Marekani zinazokwama kila mwaka katika mnyororo wa usafirishaji wa Afrika Mashariki.

Viongozi wa pande zote walisisitiza umuhimu wa mifumo ya kisheria wezeshi na ubunifu wa kifedha na usafirishaji ili kufungua ukwasi, kupunguza gharama na vikwazo vya kiutendaji, na kuwawezesha wafanyabiashara wadogo na wa kati, ambao ndio uti wa mgongo wa sekta ya usafirishaji.




Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila, akizungumza na Mjumbe wa Bodi ya Viaservice – Asiye Mtendaji,Bw. Abdulsamad Abdulrahim, baada ya ziara katika ofisi za Benki Kuu jijini Dar es Salaam tarehe 25 Agosti 2025.

# NAIBU GAVANA BOT ARIDHISHWA NA USHIRIKI WA BENKI KUU NANENANE



Naibu Gavana, Bw. Julian Banzi Raphael, akizungumza jambo kuhusu uchumi wa Tanzania alipofanya ziara katika banda la Benki Kuu kwenye Maonesho ya Nanenane. Kutoka kulia ni Meneja Msaidizi, Idara ya Mawasiliano BoT, Bi. Noves Moses, Afisa Mkuu Mwandamizi wa Itifaki, Bw. Malkias Mombo, Wachumi, Bw. Ladslaus Syldion na Bi. Hossana Mpango.

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) anayeshughulikia masuala ya Utawala na Udhibiti wa Ndani, Bw. Julian Banzi Raphael, ametembelea banda la Benki Kuu ya Tanzania katika Maonesho ya Wakulima – Nanenane yaliyofanyika kitaifa katika viwanja vya Nanenane, jijini Dodoma, kuanzia tarehe 1 hadi 8 Agosti 2025.

Katika ziara hiyo, Bw. Raphael alipokelewa na Meneja Msaidizi, Idara ya Mawasiliano BoT, Bi. Noves Moses, na kupewa maelezo ya kina na wataalamu wa BoT kuhusu namna wanavyotoa elimu kwa wananchi juu ya majukumu ya msingi ya Benki Kuu.

Bw. Raphael alieleza kuridhishwa kwake na maandalizi ya Benki Kuu katika maonesho hayo na kusisitiza umuhimu wa kuendelea kutoa elimu kwa umma ili kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya fedha na mchango wa Benki Kuu katika uchumi wa taifa.

Awali, Naibu Gavana huyo alitembelea pia banda ya Bodi ya Bima ya Amana (DIB) pamoja na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), ambapo alipata fursa ya kujionea huduma mbalimbali zinazotolewa na taasisi hizo.





Naibu Gavana, Bw. Julian Banzi Raphael, akizungumza jambo kuhusu mifumo ya malipo alipofanya ziara katika banda la Benki Kuu kwenye Maonesho ya Nanenane jijini Dodoma. Kutoka kulia Meneja Msaidizi, Idara ya Mawasiliano BoT, Bi. Noves Moses, Meneja Uendeshaji, Bodi ya Bima ya Amana (DIB), Bw. Nkamwa Magina, Afisa Mkuu Mwandamizi wa Itifaki, Bw. Malkias Mombo, Wahasibu kutoka Kurugenzi ya Usimamizi wa Mifumo ya Malipo ya Taifa, CPA. Edgar Mwakasitu na Bi. Lydia Malima.

# BOT MBEYA MSHINDI WA KWANZA NANENANE NYANDA ZA JUU KUSINI

Tawi la Benki Kuu Mbeya limeibuka mshindi wa kwanza katika Maonesho ya Nanenane Nyanda za Juu Kusini kutokana na huduma bora walizozitoa.

BoT Mbeya ilikabidhiwa tuzo kuashiria ushindi huo Agosti 8, 2025 siku ya kilele cha sikukuu ya Nanenane katika Viwanja vya Nanenane, John Mwakangale jijini Mbeya.

Zawadi hiyo ilitolewa na Kaimu Mkuu Mkoa wa Arusha Mhe. Makongoro Nyerere ambaye alijionea huduma zinazotolewa na wataalamu wa Benki Kuu kwa wananchi wanaotembelea banda letu.

Ushindi huo unathibitisha jitihada za Benki Kuu katika kutoa elimu kwa wananchi, ili kuwajengea uelewa kuhusu masuala ya fedha na kuhimiza matumizi ya taasisi rasmi za fedha kwa lengo la kunufaika na huduma kama vile uwekaji akiba, uwekezaji na mikopo.



Kutoka kushoto ni Meneja Idara ya Uchumi BoT Mbeya, Bi. Joyce Kivamba, Meneja Idara ya Fedha na Utawala BoT Mbeya, Bi. Maristella Kamuzora, Mkurugenzi wa Tawi la Benki Kuu Mbeya, Dkt. James Machemba, Meneja Idara ya Uendeshaji BoT Mbeya, Bi. Graceana Bemeye na Meneja Msaidizi Idara ya Uchumi BoT Mbeya, Dkt. Ulrick Mumburi.



Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Mhe. Makongoro Nyerere, akimkabidhi Mkurugenzi wa Tawi la Benki Kuu Mbeya, Dkt. James Machemba, Tuzo ya mshindi wa kwanza wa jumla katika Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

# KIFAHAMU KIKOKOTOO CHA MIKOPO NA FAIDA ZAKE

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imezindua huduma mpya ya kidigitali ya Kikokotoo cha Mikopo, kinachopatikana kupitia tovuti yake, ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakopaji.

Huduma hii inamwezesha mtumiaji kukadiria kiwango cha marejesho ya mkopo kila mwezi, kuelewa athari za mabadiliko ya viwango vya riba, na kupanga matumizi yake ya kifedha kwa ufanisi zaidi.

Kwa kutumia kikokotoo hiki, wananchi wanaweza kuingiza aina ya mkopo, kiasi wanachohitaji, tarehe ya kuanza mkopo na vipindi vya malipo ili kupata makadirio ya marejesho.

Benki Kuu imechukua hatua hatua hii ili kuongeza uelewa wa kifedha na kusaidia wateja kufanya maamuzi sahihi kabla ya kukopa.

Huduma hii inapatikana moja kwa moja kupitia simu au kompyuta, ikirahisisha kupanga bajeti na kuhakikisha usalama wa kifedha kwa wakopaji nchini.

**Faida za kutumia kikokotoo cha BoT**

• Makadirio Sahihi ya Marejesho
Kikokotoo kinakuwezesha kujua kiwango cha malipo ya kila mwezi kabla ya kukopa, hivyo unajipanga mapema.

• Uelewa wa Viwango vya Riba
Unapata mwanga kuhusu jinsi riba inavyoathiri deni lako, na unaweza kulinganisha mikopo yenye masharti tofauti.

• Mipango Bora ya Fedha
Unapanga bajeti yako kwa ufanisi kwa kujua gharama kamili za mkopo na muda wa kulipa.

• Kuepuka Mzigo wa Deni
Kwa taarifa sahihi, unaweza kuchagua mkopo unaokidhi uwezo wako, hivyo kupunguza hatari ya kushindwa kulipa.

• Upatikanaji wa Haraka na Rahisi
Huduma inapatikana mtandaoni kupitia simu au kompyuta muda wowote, bila gharama.

• Kutoa Uamuzi wa Kifedha Ulio Sahihi
Hukupa msingi wa kufanya maamuzi ya busara kabla ya kuingia mkataba wa mkopo.






# ULINGANISHO WA KINA WA ADA NA GHARAMA ZINAZOTOZWA NA BENKI

Takwimu hizi zinatoa ulinganisho wa kina wa ada na gharama zinazotozwa kwa wateja binafsi katika benki na taasisi mbalimbali za fedha zlnazosimamiwa na kudhibitiwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Ada na gharama hizi zimegawanywa katika maeneo Matano ambayo ni kufungua akaunti, ada za usimamizi wa akaunti za kila mwezi, hati za taarifa za akaunti, ada za mikopo, na Ada za Utoaji Fedha Kupitia ATM. Ada hizi, gharama na viwango vinavyohusiana vimechapishwa hapa kwa kumbukumbu ya masahihisho ya tarehe 4 Septemba 2025.

## 1. Kiasi cha Chini cha Kufungua Akaunti

| Na. | Maelezo | Akaunti ya Akiba | Akaunti ya Hundi |
|---|---|---|---|
| | Benki — Bakaa/Salio | Kiasi cha Chini cha Kufungua Akaunti | Kiasi cha Chini cha Kufungua Akaunti |
| 1. | Absa Bank Tanzania Limited | 0 | 0 |
| 2. | Access Bank Tanzania Ltd | 20,000 | 10,000 |
| 3. | Akiba Commercial Bank Plc | 15,000 | 100,000 |
| 4. | Amana Bank Limited | 20,000 | 0 |
| 5. | Azania Bank Public Limited Company | 0 | 0 |
| 6. | Bank of Africa Tanzania Limited | 5,000 | 20,000 |
| 7. | Bank of Baroda Tanzania Limited | 20,000 | 200,000 |
| 8. | Bank of India Tanzania Limited | 50,000 | 200,000 |
| 9. | China Dasheng Bank Limited | 20,000 | 50,000 |
| 10. | Citibank Tanzania Limited | HAIPO | HAIPO |
| 11. | Co-operative Bank Tanzania Limited | 5,000 | 50,000 |
| 12. | CRDB Bank Plc | 0 | 0 |
| 13. | DCB Commercial Bank Plc | 20,000 | 50,000 |
| 14. | Diamond Trust Bank Tanzania Plc | 5,000 | 50,000 |
| 15. | Ecobank Tanzania Limited | 0 | 3,000 |
| 16. | Equity Bank Tanzania Limited | 20,000 | 100,000 |
| 17. | Exim Bank Tanzania Limited | 5,000 | 10,000 |
| 18. | Finca Microfinance Bank Tanzania Limited | 0 | HAIPO |
| 19. | Guaranty Trust Bank Tanzania Limited | 20,000 | 20,000 |
| 20. | Habib African Bank Limited | 50,000 | 500,000 |
| 21. | I & M Bank Tanzania Limited | 10,000 | 10,000 |
| 22. | International Commercial Bank Tanzania Ltd | 0 | 50,000 |
| 23. | KCB Bank Tanzania Limited | 10,000 | 50,000 |
| 24. | Letshego Faidika Bank Tanzania Limited | 20,000 | 20,000 |
| 25. | Maendeleo Bank Plc | 0 | 50,000 |
| 26. | Mkombozi Commercial Bank Plc | 5,000 | 20,000 |
| 27. | MUCOBA Bank Plc | 0 | HAIPO |
| 28. | Mwalimu Commercial Bank Limited | 0 | 0 |
| 29. | Mwanga Hakika Bank Ltd | 20,000 | 50,000 |
| 30. | National Bank of Commerce Limited | 0 | 5,000 |
| 31. | NCBA Bank Tanzania Limited | 50,000 | 50,000 |
| 32. | NMB Bank Plc | 7,000 | 0 |
| 33. | Peoples Bank of Zanzibar Limited | 20,000 | 100,000 |
| 34. | Selcom Microfinance Bank Tanzania Limited | 0 | HAIPO |
| 35. | Stanbic Bank Tanzania Ltd | 10,000 | 5,000 |
| 36. | Standard Chartered Bank Tanzania Ltd | HAIPO | HAIPO |
| 37. | Tanzania Agricultural Development Bank Limited | HAIPO | HAIPO |
| 38. | Tanzania Commercial Bank Plc | 5,000 | 100,000 |
| 39. | TIB Development Bank Limited | HAIPO | HAIPO |
| 40. | Uchumi Commercial bank Limited | 1,000 | 100,000 |
| 41. | United Bank for Africa Tanzania Limited | 15,000 | 30,000 |
| 42. | Visionfund Tanzania Microfinance Bank Limited | 10,000 | HAIPO |

## 2. Ada ya Usimamizi kwa Mwezi

| Na. | Maelezo | | Akaunti ya Akiba | | Akaunti ya Hundi | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Benki | Ada/Gharama | Kiasi cha Chini | Kiasi cha Juu | Kiasi cha Chini | Kiasi cha Juu |
| 1. | Absa Bank Tanzania Limited | | 0 | 15,000 | 0 | 15,000 |
| 2. | Access Bank Tanzania Ltd | | 0 | 10,000 | 0 | 35,000 |
| 3. | Akiba Commercial Bank Plc | | 2,200 | 2,200 | 15,950 | 15,950 |
| 4. | Amana Bank Limited | | 2,000 | 2,000 | 0 | 15,000 |
| 5. | Azania Bank Public Limited Company | | 0 | 25,000 | 0 | 30,000 |
| 6. | Bank of Africa Tanzania Limited | | 0 | 2,300 | 0 | 30,000 |
| 7. | Bank of Baroda Tanzania Limited | | 1,900 | 1,900 | 3,700 | 3,700 |
| 8. | Bank of India Tanzania Limited | | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 9. | China Dasheng Bank Limited | | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 10. | Citibank Tanzania Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 11. | Co-operative Bank Tanzania Limited | | 2,000 | 2,000 | 10,000 | 10,000 |
| 12. | CRDB Bank Plc | | 0 | 1,770 | 0 | 4,237 |
| 13. | DCB Commercial Bank Plc | | 3,000 | 3,000 | 10,000 | 10,000 |
| 14. | Diamond Trust Bank Tanzania Plc | | 0 | 0 | 10,000 | 20,000 |
| 15. | Ecobank Tanzania Limited | | 0 | 15,000 | 0 | 20,000 |
| 16. | Equity Bank Tanzania Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 17. | Exim Bank Tanzania Limited | | 2,000 | 6,000 | 5,000 | 25,000 |
| 18. | Finca Microfinance Bank Tanzania Limited | | 1,770 | 2,360 | HAIPO | HAIPO |
| 19. | Guaranty Trust Bank Tanzania Limited | | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 20. | Habib African Bank Limited | | 0 | 0 | 35,000 | 35,000 |
| 21. | I & M Bank Tanzania Limited | | 0 | 0 | 1,000 | 50,000 |
| 22. | International Commercial Bank Tanzania Ltd | | 0 | 20,000 | 15,000 | 35,000 |
| 23. | KCB Bank Tanzania Limited | | 1,500 | 1,500 | 10,000 | 10,000 |
| 24. | Letshego Faidika Bank Tanzania Limited | | 1,000 | 1,000 | 3,000 | 3,000 |
| 25. | Maendeleo Bank Plc | | 0 | 6,000 | 2,000 | 15,000 |
| 26. | Mkombozi Commercial Bank Plc | | 0 | 10,000 | 12,000 | 18,000 |
| 27. | MUCOBA Bank Plc | | 0 | 2,000 | HAIPO | HAIPO |
| 28. | Mwalimu Commercial Bank Limited | | 0 | 1,500 | 5,000 | 7,500 |
| 29. | Mwanga Hakika Bank Ltd | | 2,500 | 2,500 | 10,000 | 10,000 |
| 30. | National Bank of Commerce Limited | | 0 | 4,000 | 800 | 15,400 |
| 31. | NCBA Bank Tanzania Limited | | 0 | 0 | 10,000 | 10,000 |
| 32. | NMB Bank Plc | | 0 | 0 | 0 | 1,800 |
| 33. | Peoples Bank of Zanzibar Limited | | 2,000 | 2,000 | 7,000 | 7,000 |
| 34. | Selcom Microfinance Bank Tanzania Limited | | 0 | 0 | 2,000 | 2,000 |
| 35. | Stanbic Bank Tanzania Ltd | | 0 | 2,000 | 0 | 10,000 |
| 36. | Standard Chartered Bank Tanzania Ltd | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 37. | Tanzania Agricultural Development Bank Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 38. | Tanzania Commercial Bank Plc | | 2,200 | 2,200 | 7,000 | 7,000 |
| 39. | TIB Development Bank Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 40. | Uchumi Commercial bank Limited | | 1,500 | 1,800 | 5,000 | 15,000 |
| 41. | United Bank for Africa Tanzania Limited | | 0 | 0 | 10,000 | 13,000 |
| 42. | Visionfund Tanzania Microfinance Bank Limited | | 1,500 | 3,000 | HAIPO | HAIPO |

## 3. Ada za Kupata Hati za Taarifa za Akaunti

| Na. | Maelezo | | Ada ya Hati ya Taarifa kupitia Kaunta | | Ada ya Hati ya Taarifa kupitia ATM | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Benki | Ada/Gharama | Kiasi cha Chini | Kiasi cha Juu | Kiasi cha Chini | Kiasi cha Juu |
| 1. | Absa Bank Tanzania Limited | | 2,500 Kwa kila ombi | 2,500 Kwa kila ombi | 1,000 Kwa kila ombi | 1,000 Kwa kila ombi |
| 2. | Access Bank Tanzania Ltd | | 2,500 Kwa kila ombi | 100,000 Kwa kila ombi | 300 Kwa kila ombi | 300 Kwa kila ombi |
| 3. | Akiba Commercial Bank Plc | | 2,500 Kwa kila ombi | 2,500 Kwa kila ombi | 400 Kwa kila ombi | 400 Kwa kila ombi |
| 4. | Amana Bank Limited | | 6,000 Kwa kila ombi | 6,000 Kwa kila ombi | 500 | 500 |
| 5. | Azania Bank Public Limited Company | | 2,500 Kwa kila ukurasa | 2,500 Kwa kila ukurasa | 0 | 0 |
| 6. | Bank of Africa Tanzania Limited | | 2,000 Kwa kila ukurasa | 100,000 Kwa kila ombi | 400 Kwa kila ombi | 600 Kwa kila ombi |
| 7. | Bank of Baroda Tanzania Limited | | 10,000 Kwa kila ombi | 10,000 Kwa kila ombi | 0 | 0 |
| 8. | Bank of India Tanzania Limited | | 1,500 Kwa kila ukurasa | 1,500 Kwa kila ukurasa | HAIPO | HAIPO |
| 9. | China Dasheng Bank Limited | | 1,100 Kwa kila ukurasa | 1,100 Kwa kila ukurasa | HAIPO | HAIPO |
| 10. | Citibank Tanzania Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 11. | Co-operative Bank Tanzania Limited | | 0 | 0 | 500 | 500 |
| 12. | CRDB Bank Plc | | 1,695 kwa kurasa 5 | 1,695 kwa kurasa 5 +500 kwa kurasa ziada | 424 Kwa kila hati | 424 Kwa kila hati |
| 13. | DCB Commercial Bank Plc | | 1,000 Kwa kila ukurasa | 1,000 Kwa kila ukurasa | 300 Kwa kila ombi | 300 Kwa kila ombi |
| 14. | Diamond Trust Bank Tanzania Plc | | 10,000 Kwa kila hati | 10,000 Kwa kila hati | 0 | 0 |
| 15. | Ecobank Tanzania Limited | | 1,000 Kwa kila ukurasa | 5,000 Kwa kila ukurasa | 650 Kwa kila muamala | 650 Kwa kila muamala |
| 16. | Equity Bank Tanzania Limited | | 2000 Kwa kila ukurasa | 2000 Kwa kila ukurasa | 400 Kwa kila ombi | 400 Kwa kila ombi |
| 17. | Exim Bank Tanzania Limited | | 2,000 Kwa kila mwezi | 5,000 Kwa kila mwezi | 1,000 Kwa kila ombi | 1,000 Kwa kila ombi |
| 18. | Finca Microfinance Bank Tanzania Limited | | 0 | 1,500 Kwa kila ukurasa | HAIPO | HAIPO |
| 19. | Guaranty Trust Bank Tanzania Limited | | 4,130 Kwa kila ukurasa | 4,130 Kwa kila ukurasa | 1,000 Kwa kila ombi | 1,000 Kwa kila ombi |
| 20. | Habib African Bank Limited | | 2,000 Kwa kila ukurasa | 2,000 Kwa kila ukurasa | HAIPO | HAIPO |
| 21. | I & M Bank Tanzania Limited | | 0 | 1,500 Kwa kila ukurasa | 0 | 0 |
| 22. | International Commercial Bank Tanzania Ltd | | 1,000 Kwa kila ukurasa | 1,000 Kwa kila ukurasa | 350 Kwa kila ombi | 350 Kwa kila ombi |
| 23. | KCB Bank Tanzania Limited | | 0 | 2,000 Kwa kila ukurasa | 0 | 0 |
| 24. | Letshego Faidika Bank Tanzania Limited | | 1,000 Kwa kila ukurasa | 1,000 Kwa kila ukurasa | 300 Kwa kila ombi | 700 Kwa kila ombi |
| 25. | Maendeleo Bank Plc | | 2,000 Kwa kila ukurasa | 2,000 Kwa kila ukurasa | 500 Kwa kila muamala | 500 Kwa kila muamala |
| 26. | Mkombozi Commercial Bank Plc | | 1,500 Kwa kila ukurasa | 1,500 Kwa kila ukurasa | 500 Kwa kila ombi | 500 Kwa kila ombi |
| 27. | MUCOBA Bank Plc | | 2,000 Kwa kila ukurasa | 2,000 Kwa kila ukurasa | 400 | 400 |
| 28. | Mwalimu Commercial Bank Limited | | 1, 500 Kwa kila ukurasa | 1, 500 Kwa kila ukurasa | HAIPO | HAIPO |
| 29. | Mwanga Hakika Bank Ltd | | 2,000 Kwa kila ombi | 2,000 Kwa kila ombi | HAIPO | HAIPO |
| 30. | National Bank of Commerce Limited | | 1,500 Kwa kila ombi | 6,500 Kwa kila ombi | 300 Kwa kila ombi | 750 Kwa kila ombi |
| 31. | NCBA Bank Tanzania Limited | | 3,000 Kwa kila ukurasa | 3,000 Kwa kila ukurasa | 400 Kwa kila ombi | 400 Kwa kila ombi |
| 32. | NMB Bank Plc | | 2,000 Kwa kila mwezi | 2,000 Kwa kila mwezi | 413 Kwa kila ombi | 413 Kwa kila ombi |
| 33. | Peoples Bank of Zanzibar Limited | | 500 Kwa kila ombi | 500 Kwa kila ombi | 400 Kwa kila ukurasa | 400 Kwa kila ukurasa |
| 34. | Selcom Microfinance Bank Tanzania Limited | | 0 | 10,000 Kwa kila hati | HAIPO | HAIPO |
| 35. | Stanbic Bank Tanzania Ltd | | 1,000 Kwa kila hati | 5,000 Kwa kila hati | 900.01 Kwa kila hati | 900.01 Kwa kila hati |
| 36. | Standard Chartered Bank Tanzania Ltd | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 37. | Tanzania Agricultural Development Bank Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 38. | Tanzania Commercial Bank Plc | | 2,000 Kwa kila ukurasa | 2,000 Kwa kila ukurasa | 400 Kwa kila ombi | 400 Kwa kila ombi |
| 39. | TIB Development Bank Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 40. | Uchumi Commercial bank Limited | | 1,500 Kwa kila hati | 1,500 Kwa kila hati | 400 | 500 |
| 41. | United Bank for Africa Tanzania Limited | | 1,000 Kwa kila ukurasa | 1,000 Kwa kila ukurasa | HAIPO | HAIPO |
| 42. | Visionfund Tanzania Microfinance Bank Limited | | 0 | 55,400 | 0 | 0 |

## 4. Ada za Utoaji Fedha Kupitia ATM

| Na. | Maelezo | | ATM ya Benki Yako | | ATM ya Benki Nyingine | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Benki | Ada/Gharama | Kiasi cha Chini | Kiasi cha Juu | Kiasi cha Chini | Kiasi cha Juu |
| 1. | Absa Bank Tanzania Limited | | 1,000 | 2,500 | 4,000 | 5,000 |
| 2. | Access Bank Tanzania Ltd | | 1,500 | 1,500 | 3,540 | 3,540 |
| 3. | Akiba Commercial Bank Plc | | 1,700 | 1,700 | 3,600 | 3,600 |
| 4. | Amana Bank Limited | | 1,800 | 2,800 | 5,000 | 5,000 |
| 5. | Azania Bank Public Limited Company | | 1,500 | 1,700 | 5,000 | 5,000 |
| 6. | Bank of Africa Tanzania Limited | | 1,700 | 2,000 | 3,500 | 4,000 |
| 7. | Bank of Baroda Tanzania Limited | | 0 | 0 | HAIPO | HAIPO |
| 8. | Bank of India Tanzania Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 9. | China Dasheng Bank Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 10. | Citibank Tanzania Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 11. | Co-operative Bank Tanzania Limited | | 1,500 | 1,900 | 4,000 | 4,000 |
| 12. | CRDB Bank Plc | | 1,017 | 3,390 | 4,000 | 4,000 |
| 13. | DCB Commercial Bank Plc | | 1,700 | 1,700 | 3,000 | 3,000 |
| 14. | Diamond Trust Bank Tanzania Plc | | 1,200 | 1,200 | 3,000 | 3,000 |
| 15. | Ecobank Tanzania Limited | | 1,000 | 1,600 | 2,500 | 6,000 |
| 16. | Equity Bank Tanzania Limited | | 400 | 1,600 | 4,500 | 4,500 |
| 17. | Exim Bank Tanzania Limited | | 1,300 | 1,800 | 3,540 | 3,540 |
| 18. | Finca Microfinance Bank Tanzania Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 19. | Guaranty Trust Bank Tanzania Limited | | 1,500 | 1,500 | 2,360 | 2,360 |
| 20. | Habib African Bank Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 21. | I & M Bank Tanzania Limited | | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 |
| 22. | International Commercial Bank Tanzania Ltd | | 1,500 | 1,700 | 2,000 | 2,000 |
| 23. | KCB Bank Tanzania Limited | | 1,000 | 1,000 | 2,500 | 2,500 |
| 24. | Letshego Faidika Bank Tanzania Limited | | 1,500 | 4,500 | 4,720 | 4,720 |
| 25. | Maendeleo Bank Plc | | 1,300 | 1,300 | HAIPO | HAIPO |
| 26. | Mkombozi Commercial Bank Plc | | 1,500 | 1,700 | 2,000 | 2,200 |
| 27. | MUCOBA Bank Plc | | 1,500 | 4,000 | 4,000 | 4,000 |
| 28. | Mwalimu Commercial Bank Limited | | 1,500 | 1,700 | 2,200 | 3,000 |
| 29. | Mwanga Hakika Bank Ltd | | 1,500 | 1,700 | 3,500 | 3,500 |
| 30. | National Bank of Commerce Limited | | 1,500 | 4,000 | 3,000 | 5,000 |
| 31. | NCBA Bank Tanzania Limited | | 1,700 | 1,700 | 3,500 | 3,500 |
| 32. | NMB Bank Plc | | 1,100 | 1,800 | 3,540 | 3,540 |
| 33. | Peoples Bank of Zanzibar Limited | | 1,700 | 1,700 | 4,000 | 4,000 |
| 34. | Selcom Microfinance Bank Tanzania Limited | | 2,500 | 2,500 | 2,500 | 2,500 |
| 35. | Stanbic Bank Tanzania Ltd | | 1,400 | 3,000 | 3,000 | 5,000 |
| 36. | Standard Chartered Bank Tanzania Ltd | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 37. | Tanzania Agricultural Development Bank Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 38. | Tanzania Commercial Bank Plc | | 1,800 | 1,800 | 4,000 | 4,000 |
| 39. | TIB Development Bank Limited | | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 40. | Uchumi Commercial bank Limited | | 1,500 | 1,700 | 1,500 | 1,700 |
| 41. | United Bank for Africa Tanzania Limited | | 1,000 | 1,500 | 1,700 | 8,000 + 1% |
| 42. | Visionfund Tanzania Microfinance Bank Limited | | HAIPO | HAIPO | 1,200 | 4,000 |

## 5. Ada za Mikopo na Kiwango cha Riba cha Mwaka

| Na. | Maelezo | Ada ya Usimamizi | | Ada ya Kujidhatiti Kuchukua Mkopo | | Ada ya Kuboresha Mkopo | | Ada ya Marekebisho ya Vigezo na Masharti | | Kiwango cha Riba | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Benki / Ada/Gharama | Kiasi cha Chini | Kiasi cha Juu | Kiasi cha Chini | Kiasi cha Juu | Kiasi cha Chini | Kiasi cha Juu | Kiasi cha Chini | Kiasi cha Juu | Kiasi cha Chini | Kiasi cha Juu |
| 1. | Absa Bank Tanzania Limited | 0.75% | 1.75% | 0 | 0 | 1% | 1% | 0 | 0 | 7% | 20% |
| 2. | Access Bank Tanzania Ltd | 1% | 2% | 1% | 2% | 0 | 2% | 0 | 2% | 15% | 21.50% |
| 3. | Akiba Commercial Bank Plc | 2% | 4% | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14% | 24% |
| 4. | Amana Bank Limited | 0 | 0 | 0 | 0 | 1% | 1% | 0 | 0 | 0 | 48% |
| 5. | Azania Bank Public Limited Company | 1.50% | 2.50% | HAIPO | HAIPO | 0 | 0 | 1% | 1% | 18% | 18% |
| 6. | Bank of Africa Tanzania Limited | 1% | 1% | 2% | 2% | Makubaliano | Makubaliano | Makubaliano | Makubaliano | 17% | 17% |
| 7. | Bank of Baroda Tanzania Limited | 24,400 | 24,400 | 1.32% | 1.32% | 1.82% | 1.82% | 1.20% | 1,000,000 | 15% | 20% |
| 8. | Bank of India Tanzania Limited | 0 | 0 | 0 | 0 | 1.50% | 1.50% | 0.25% | 0.25% | 15.50% | 20.5% |
| 9. | China Dasheng Bank Limited | 1.10% | 1.10% | 0 | 0 | 1.10% | 1.10% | 1.10% | 1.10% | 16% | 16% |
| 10. | Citibank Tanzania Limited | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 11. | Co-operative Bank Tanzania Limited | 100,000 | 2.5% | 1% | 1% | HAIPO | HAIPO | 100,000 | 1% | 10% | 23% |
| 12. | CRDB Bank Plc | 1.25% | 1.25% | 0.5% | 0.5% | 1.25% | 1.25% | 1.25% | 1.25% | 0 | 16% |
| 13. | DCB Commercial Bank Plc | 0.50% | 1,000,000 | 3% | 3% | Makubaliano | Makubaliano | Makubaliano | Makubaliano | 19% | 19% |
| 14. | Diamond Trust Bank Tanzania Plc | 1% | 3% | 1% | 1% | 1% | 1% | 1.10% | 1.10% | 20% | 20% |
| 15. | Ecobank Tanzania Limited | 0 | 0 | 0 | 0 | 1.5% | 2.5% | 0 | 0 | 15% | 20% |
| 16. | Equity Bank Tanzania Limited | 1% | 3% | 0 | 0 | 1% | 2% | 1% | 1% | 15% | 25% |
| 17. | Exim Bank Tanzania Limited | 0 | 0 | 1% | 2% | 1.12% | 1.12% | 1.12% | 1.12% | Inategemea Soko | Inategemea Soko |
| 18. | Finca Microfinance Bank Tanzania Limited | 0% | 3% | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 24% | 60% |
| 19. | Guaranty Trust Bank Tanzania Limited | 1% | 1% | 2% | 2% | HAIPO | HAIPO | 2% | 2% | 17% | 17% |
| 20. | Habib African Bank Limited | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | 0.25% | 1.50% | 0 | 0 | 10% | 27.25% |
| 21. | I & M Bank Tanzania Limited | 1.10% | 1.10% | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 21% | 21% |
| 22. | International Commercial Bank Tanzania Ltd | 2% | 2% | 1% | 1% | 2% | 2% | 1% | 1% | 20% | 20% |
| 23. | KCB Bank Tanzania Limited | 2.40% | 2.40% | 2.40% | 2.40% | 2.40% | 2.40% | 2.40% | 2.40% | 19% | 19% |
| 24. | Letshego Faidika Bank Tanzania Limited | 1% | 2% | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8% | 48% |
| 25. | Maendeleo Bank Plc | 1% | 3% | 0 | 0 | 1% | 1% | 1% | 3% | 18% | 24% |
| 26. | Mkombozi Commercial Bank Plc | 2.50% | 2.50% | 1.20% | 1.20% | 0 | 0 | 0 | 0.5% | 17% | 25% |
| 27. | MUCOBA Bank Plc | 1% | 2% | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | 10% | 30% |
| 28. | Mwalimu Commercial Bank Limited | 1.5% | 3.5% | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14% | 18% |
| 29. | Mwanga Hakika Bank Ltd | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | 1% | 3.5% | 0.5% | 0.5% | Makubaliano | Makubaliano |
| 30. | National Bank of Commerce Limited | 0 | 0 | 0 | 0 | 0.50% | 2% | 0 | 0 | 13% | 22% |
| 31. | NCBA Bank Tanzania Limited | 0 | 0 | 0 | 0 | 0.50% | 2% | 0 | 0 | 21% | 21% |
| 32. | NMB Bank Plc | 1.00% | 1.80% | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14% | 14% |
| 33. | Peoples Bank of Zanzibar Limited | 0 | 0 | 0 | 0 | 2% | 2% | 0 | 0 | 16% | 16% |
| 34. | Selcom Microfinance Bank Tanzania Limited | 3.40% | 3.40% | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6% | 33.6% |
| 35. | Stanbic Bank Tanzania Ltd | 0 | 0 | 2% | 2% | 2% | 2% | 0 | 0 | 17% | 17% |
| 36. | Standard Chartered Bank Tanzania Ltd | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO |
| 37. | Tanzania Agricultural Development Bank Limited | 0.50% | 1.50% | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | HAIPO | 8% | 13% |
| 38. | Tanzania Commercial Bank Plc | 1.50% | 1.50% | 20,000 | 20,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14% | 17% |
| 39. | TIB Development Bank Limited | HAIPO | HAIPO | 2.36% | 2.36% | 5,000,000 | 0.097% (mkopo zaidi ya Bn. 1) | 0.65% | 0.65% | 13% | 20.2% |
| 40. | Uchumi Commercial bank Limited | 0 | 2% | HAIPO | HAIPO | 0 | 2% | HAIPO | HAIPO | 14% | 21% |
| 41. | United Bank for Africa Tanzania Limited | 1% | 2% | 2% | 2% | 0 | 0 | 16% | 16% | 16% | 16% |
| 42. | Visionfund Tanzania Microfinance Bank Limited | 2.50% | 4.4% | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 30% | 60% |

# BOT YAIKARIBISHA ABSA GROUP KUENDELEA KUWEKEZA TANZANIA



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, ameikaribisha Absa Group kupitia kampuni zake kuendelea kuwekeza katika sekta ya fedha nchini.

Aliyasema hayo Jumanne Julai 22, 2025 alipokutana na kufanya mazungumzo na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Absa Group, Bw. Kenny Fihla katika ofisi ndogo za Makao Makuu ya Benki Kuu jijini Dar es Salaam.

Kuhusu kuwekeza katika sekta ya fedha, Gavana Tutuba amesema; "Tanzania kuna mazingira rafiki ya kufanyia biashara na kuendelea kuimarika kwa uchumi wa Tanzania.

"Ripoti kutoka Kampuni ya Kimataifa Inayojihusisha na Kufanya Tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa ya Fitch Ratings inaonesha Tanzania ipo katika daraja la B+ ikiononesha mwenendo mzuri wa uchumi,"ameongeza Gavana Tutuba.

Kwa upande wake, Afisa Mtendaji Mkuu wa Absa Group, Bw. Fihla ambaye ameteuliwa hivi karibuni ameipongeza Benki Kuu kwa usimamizi thabiti wa sekta ya fedha na uchumi wa nchi kiujumla. Absa Group kwa Tanzania inamiliki hisa nyingi katika Benki ya NBC.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Naibu Gavana (Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha),Bi. Sauda Msemo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Bw. Theobald Sabi na Mkurugenzi Mtendaji wa Absa Group kwa ukanda wa Afrika, Saviour Chibiya.



Gavana Emmanuel Tutuba na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Absa Group, Bw. Kenny Fihla wakizungumza baada ya kikao kilichofanyika katika ofisi za Benki Kuu jijini Dar es Salaam tarehe 22 Julai, 2025.



# BOT ACADEMY NA WFP WAUNGANA KUWAJENGEA VIJANA UWEZO WA ELIMU YA FEDHA

Chuo cha Benki Kuu ya Tanzania (BoT Academy) kimesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa lengo la kuwajengea uwezo wa elimu ya fedha vijana kupitia Mradi wa Vijana Kilimo Biashara (VKB).

Hafla hii ya utiaji saini ilifanyika Julai 31, 2025, katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam ambapo mgeni rasmi alikuwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba.

Akizungumza katika hafla hiyo, Gavana Tutuba ameishukuru na kuipongeza WFP kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kuwawezesha vijana wanufaika wa mradi huo kupata maarifa ya kifedha yanayowawezesha kuboresha maisha yao kupitia kilimo biashara.

"Leo tumesaini rasmi ushirikiano wa Mradi wa Vijana Kilimo Biashara, ambao unatekelezwa kwa pamoja na BoT Academy Mwanza na WFP. Wenzetu wa WFP wamekubali kufadhili masuala ya elimu ya fedha kwa vijana katika mikoa saba hapa nchini. Mikoa hiyo ni Dodoma, Arusha, Tabora, Singida, Manyara, Simiyu na Shinyanga." amesema Gavana Tutuba.

Ameeleza kuwa Chuo cha Benki Kuu kitatoa elimu ya fedha kwa vijana ambao watawezeshwa na WFP kupitia mradi wa VKB ili waweze kusimamia fedha zao kwa ueledi na kutumia mifumo rasmi ya kifedha.

Gavana Tutuba ameongeza kuwa kwa kufanya hivyo vijana ambao wamepewa elimu hiyo wataweza kufanya shughuli zao za kilimo kwa kujikita zaidi kwenye uzalishaji bora wenye tija kupitia kilimo cha mboga mboga, mtama pamoja na alizeti.

Aidha, Gavana Tutuba amebainisha kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha elimu ya fedha inawafikia makundi yote ya jamii, wakiwemo wanawake, watu wenye ulemavu, wavuvi, na wajasiriamali wadogo ambao utafiti unaonesha makundi hayo hayajafikiwa na elimu ya fedha ya kutosha.

Kwa upande wake, Naibu Mkurugenzi Mkazi wa WFP nchini, Bi. Christine Mendes amesema Mradi wa VKB, unaofadhiliwa na Mastercard Foundation, unalenga kuwapatia vijana wakulima ujuzi na rasilimali muhimu ili kuboresha uzalishaji na kukuza uchumi endelevu.

Bi. Mendes amesema tangu kuanza kwa mradi huo mwaka 2022, zaidi ya vijana 83,000 wameshanufaika – asilimia 70 kati yao wakiwa wanawake.

Ameongeza kuwa lengo ni kuwafikia jumla ya vijana 115,000 ifikapo mwaka 2027, huku kupitia ushirikiano huo, WFP ikitoa ufadhili wa dola za Marekani 100,000 (sawa na zaidi ya shilingi milioni 250) kwa ajili ya mafunzo ya usimamizi wa fedha, kuweka akiba, kupanga bajeti na uwekezaji wa kilimo chenye tija.




Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba (Katikati), Naibu Mkurugenzi Mkazi wa WFP nchini, Bi. Christine Mendes (wa pili kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo cha Benki Kuu na Naibu Gavana wa BoT, Bw. Julian Raphael (wa pili kulia) na Mkuu wa Chuo cha Benki Kuu, Dkt. Nicas Yabu (wa kwanza kulia) wakionesha Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Benki Kuu na WFP inayolenga kuwajengea uwezo wa elimu ya fedha vijana kupitia Mradi wa Vijana Kilimo Biashara.





# ZIARA YA KIELIMU: MINAKI NA DAR ES SALAAM SEKONDARI WATEMBELEA BOT

Wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Minaki na Shule ya Sekondari Dar es Salaam Agosti 21, 2025 walitembelea Benki Kuu ya Tanzania (BoT) jijini Dar es Salaam, ambapo walipata fursa ya kujifunza kwa undani kuhusu majukumu ya Benki Kuu katika kusimamia uchumi wa nchi na utekelezaji wa Sera ya Fedha.

Katika mafunzo waliyopatiwa, wanafunzi walielimishwa juu ya umuhimu wa kuweka akiba, nidhamu ya kifedha na fursa mbalimbali za uwekezaji zinazopatikana ndani ya sekta ya fedha. Elimu hiyo imelenga kuwajengea uelewa wa mapema kuhusu masuala ya fedha na mchango wake katika maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Vilevile, wanafunzi hao walitembelea Makumbusho ya Benki Kuu, ambapo walipata historia ya fedha nchini Tanzania, kuanzia matumizi ya mifumo ya jadi ya biashara ya kubadilishana bidhaa, kuanzishwa kwa sarafu na noti za kwanza, hadi mageuzi makubwa ya kifedha yaliyotekelezwa katika nyakati tofauti. Pia walijifunza namna majukumu ya Benki Kuu yamepanuka tangu kuanzishwa kwake, sambamba na mageuzi ya sekta ya fedha nchini.



Afisa Uhusiano wa Umma kutoka Benki Kuu, Bw. Daniel Mlimuka, akifafanua jambo kwa wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Minaki na Shule ya Sekondari Dar es Salaam walipotembelea Makumbusho ya Benki Kuu jijini Dar es Salaam.




Afisa Uhusiano wa Umma kutoka Benki Kuu, Bi. Graciana Mahega, akifafanua jambo kwa wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Minaki na Shule ya Sekondari Dar es Salaam walipotembelea Makumbusho ya Benki Kuu jijini Dar es Salaam.

# RIPOTI YA SADC YATHIBITISHA UTULIVU WA UCHUMI WA TANZANIA





Magavana wa Benki Kuu za SADC waliohudhuria mkutano wa 61 wa CCBG uliofanyika Gaborone, Botswana tarehe 11 Septemba 2025.



Mkutano wa 61 wa Kamati ya Magavana wa Benki Kuu (CCBG) za SADC, uliofanyika Gaborone, Botswana tarehe 11 Septemba 2025.

Tanzania imeendelea kuonesha utendaji imara wa uchumi mkuu ndani ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kwa mujibu wa ripoti ya kikanda iliyojadiliwa katika Mkutano wa 61 wa Kamati ya Magavana wa Benki Kuu (CCBG) za SADC, uliofanyika Gaborone, Botswana tarehe 11 Septemba 2025.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba, alihudhuria mkutano huo pamoja na magavana wenzake kutoka nchi wanachama wa SADC.

Ripoti hiyo inaonesha kuwa uchumi wa SADC ulipungua kasi ya ukuaji hadi asilimia 3.0 mwaka 2024 kutoka asilimia 3.8 mwaka 2023, huku nchi wanachama zikionesha mwenendo tofauti wa ukuaji. Tanzania iliibuka kuwa miongoni mwa nchi zilizofanya vizuri zaidi, ikisajili ukuaji wa asilimia 5.5, wa pili kwa kasi zaidi katika kanda, unaochochewa na shughuli thabiti za kiuchumi ndani ya nchi.

Kuhusu mfumuko wa bei, ingawa wastani wa kikanda ulipungua hadi asilimia 9.0 mwaka 2024 kutoka asilimia 9.5 mwaka 2023, nchi nyingi za SADC zilibaki juu ya lengo la ulinganifu wa makroekonomia la asilimia 3% – 7%. Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi saba—pamoja na Eswatini, Lesotho, Mauritius, Msumbiji, Namibia na Afrika Kusini—zilizofanikiwa kudhibiti mfumuko wa bei ndani ya kiwango kinachokubalika.

Kwa upande wa biashara, ripoti ilibainisha kuwa nchi nyingi za SADC ziliendelea kuwa waagizaji wa bidhaa kutoka nje. Hata hivyo, Tanzania ilijipambanua kwa kurekodi ziada ya biashara yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 2, ikionyesha ufanisi mkubwa wa mauzo ya nje na mchango chanya katika ushirikiano wa kibiashara wa kikanda.

Kielelezo cha Muunganiko wa Uchumi Mkuu wa SADC pia kilithibitisha nafasi ya Tanzania kama moja ya nchi zinazofanya vizuri katika kudumisha utulivu wa uchumi mwaka hadi mwaka.

Mkutano wa 61 wa Kamati ya Magavana wa Benki Kuu (CCBG) za SADC ulioongozwa na Mwenyekiti wa kamati hiyo ambaye pia ni Gavana wa Benki Kuu ya Afrika Kusini, Bw. Lesetja Kganyago, uliwapa fursa viongozi hao kujadiliana masuala mbalimbali ya kimkakati yanayolenga kuchochea ukuaji wa uchumi, kuimarisha usimamizi wa mabenki na utulivu wa sekta ya fedha, pamoja na maendeleo katika mifumo ya malipo.

# BENKI KUU NIGERIA YAPUNGUZA RIBA BAADA YA MIAKA MITANO



Benki kuu ya Nigeria (CBN) imepunguza riba yake ya kukopesha (Central Bank Rate - CBR) kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2020, hatua inayolenga kuchochea ukuaji wa uchumi.

CBN imepunguza kiwango hiko kwa pointi 50 za msingi (bps) kutokana na kupungua kwa mfumuko wa bei katika nchi hiyo hasa siku za hivi karibuni.

Kutokana na kupungua huko kwa CBR, pia Riba ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu ya Nigeria imekuwa asilimia 27 ikilinganishwa na asilimia 27.5 ya robo mwaka uliopita.

Gavana wa CBN, Olayemi Cardoso alisema; "Kupunguzwa kwa viwango vya riba hizo kulitabiriwa kutokana na kushuka kwa mfumuko wa bei kwa mwaka mzima na hitaji la kusaidia uchumi."

Mfumuko wa bei nchini humo umeendelea kupungua kwa miezi mitano mfululizo ambapo Julai ulikuwa asilimia 21.88 huku Agosti ukishuka hadi asilimia 20.12.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Reuters, Kupungua kwa Riba ya Benki Kuu kua faida mbalimbali katika kuchochea uchumi wa nchi ikiwemo mikopo ya benki za biashara kuwa nafuu

"Mabenki ya biashara hupunguza viwango vya riba kwa wateja, hivyo watu binafsi na kampuni hukopa kwa gharama ndogo.

"Kuongezeka kwa Uwekezaji; Gharama ndogo za mikopo huwahamasisha wafanyabiashara kuwekeza katika miradi mipya, kukuza ajira na uzalishaji"

"Kuchochea Matumizi ya Wateja; Watumiaji wanakopa zaidi kwa ajili ya makazi, elimu, au matumizi mengine, hivyo kuongeza mzunguko wa fedha kwenye uchumi, Kukuza Ukuaji wa Uchumi; Uwekezaji na matumizi zaidi huchangia kuongeza pato la taifa (GDP) na kuimarisha biashara."

Wachambuzi wa masuala ya fedha wanasema kupungua kwa mfumuko wa bei na kupunguzwa kwa riba ni dalili chanya kwa uchumi wa Nigeria, ingawa wameshauri kuendelea kwa nidhamu ya kifedha na ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha thamani ya Naira na bei za bidhaa muhimu hazitetereki.

Hatua hii ya CBN inaangaliwa pia kama ishara ya kujiamini kwa mamlaka za fedha kwamba uchumi wa Nigeria unaweza kuhimili kasi mpya ya ukuaji bila kurudi katika hali ya mfumuko wa bei wa juu ulioshuhudiwa miaka iliyopita.

# Benki Kuu Inang'ara

Anga za kimataifa, Benki Kuu inangára,
Huko wanafanya dhifa, vile imefanya bora,
Ni kwa mengi maarifa, kazi na kumwaga sera,
Kwa huduma jumuishi, vema tunatambuliwa.

Imepata tuzo kuu, kwa kufanya kazi bora,
Kwenye AFI iko juu, maendeleo ishara,
Ni mkutano mkuu, zajieleza Ankara,
Kwa huduma jumuishi, vema tunatambuliwa.

Benki Kuu ubunifu teknolojia bora,
Tanzania waisifu, kwa uongozi imara,
Huduma zetu nadhifu, siyo za watu kukera,
Kwa huduma jumuishi, vema tunatambuliwa.

Ushindi wa Benki Kuu, kwa ubunifu yangára,
TIPS imekuja juu, kwa malipo si mpira,
Mifumo yetu nukuu, kwa malipo TANQR,
Kwa huduma jumuishi, vema tunatambuliwa.

Benki Kuu yaongoza, sasa Tanzania bora,
Kuanzisha imeweza, kuyaweka mazingira,
Kwa Fintech kuchagiza, huduma za fedha bora,
Kwa huduma jumuishi, vema tunatambuliwa.

Jinsi yajali wateja, Benki Kuu inangára,
Wale wanaleta hoja, huduma zinapokera,
Njia ni nyingi za haja, tena zisizo hasara,
Kwa huduma jumuishi, vema tunatambuliwa.

Wewe kiswaswadu chako, Sema na BoT bora,
Hata simujanja yako, andiko linalokera,
Tapata majibu yako, mema sawa na ijara,
Kwa huduma jumuishi, vema tunatambuliwa.

Kwa huduma jumuishi, visiwani hata bara,
Benki Kuu kwa utashi, kwa kweli yafanya bora,
Hata wake watumishi, watambulika ubora,
Kwa huduma jumuishi, vema tunatambuliwa.

Lengo lake Benki Kuu, huduma za fedha bora,
Tanzania iwe juu, toka Kyela hadi Mara,
Matumizi yawe juu, kwenye bora mazingira,
Kwa huduma jumuishi, vema tunatambuliwa.

***Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)***
***lwagha@gmail.com***
***0767223602***

**Limetolewa na Idara ya Mawasiliano**
**Benki Kuu ya Tanzania**

---

Anuani:
**Barabara ya 16 ya Jakaya Kikwete, 40184**
**S.L.P. 2303 Dodoma, Tanzania**
Barua pepe:
**botcommunications@bot.go.tz**
**info@bot.go.tz**
Tovuti:
**www.bot.go.tz**